

**HOTUBA YA WAZIRI WA UCHUKUZI, MHE.
SAMUEL J. SITTA (MB), AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA
MWAKA 2015/2016**

YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI.....	1
2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA 2014/2015.....	4
2.1 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MATOKEO MAKUBWA SASA (BIG RESULTS NOW – BRN) KATIKA MWAKA 2014/2015.....	6
2.1.1 Utekelezaji wa BRN Katika Sekta ya Bandari.....	6
2.1.2 Utekelezaji wa BRN Katika Sekta ya Reli.....	9
2.2 HUDUMA ZA UCHUKUZI KWA NJIA YA NCHI KAVU.....	17
2.2.1 Usafiri na Uchukuzi kwa Njia ya Barabara...	17
2.3.2 Huduma za Usafiri na Uchukuzi Mikoani na Vijijini.....	19
2.3.3 Huduma za Usafiri Mijini.....	20
2.3.4 Huduma za Usafiri wa Reli Jijini Dar es Salaam.....	20
2.3 Usafiri na Uchukuzi kwa Njia ya Reli.....	22
2.4 Udhhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini.....	30
2.5 Udhhibiti wa Huduma za Usafiri wa Reli.....	30

2.6 Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa Njia ya Barabara.....	31
2.7 Udhibiti wa Usalama wa Vyombo vya Usafiri Majini.....	34
3.0 USAFIRI NA UCHUKUZI MAJINI.....	35
3.1 Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa.....	35
3.2 Huduma za Uchukuzi Baharini.....	39
3.3 Huduma za Bandari.....	39
4.0 USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA.....	48
4.1 Udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga.....	48
4.2 Huduma za Viwanja vya Ndege.....	56
4.3 Huduma za Usafiri wa Ndege.....	63
5.0 HUDUMA ZA HALI YA HEWA.....	65
6.0 TAASISI ZA MAFUNZO.....	69
6.1 Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI).....	69
6.2 Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).....	71
6.3 Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC).....	73
6.4 Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma.....	74
6.5 Chuo cha Reli Tabora (TIRTEC).....	74
7.0 MASUALA MTAMBUKA.....	75
7.1 Kuzingatia Masuala ya Jinsia.....	75

7.2 Utunzaji wa Mazingira.....	76
7.3 Usalama katika sekta ya uchukuzi.....	79
7.4 Udhibiti wa UKIMWI.....	81
7.5 Mapambano Dhidi ya Rushwa.....	82
7.6 Habari, Elimu na Mawasiliano.....	82
8.0 MALENGO YA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KATIKA MWAKA 2015/2016.....	85
8.1 Miradi Itakayotekelezwa Katika Mwaka 2015/2016 Chini ya Mpango wa BRN.....	85
8.2 Miradi Itakayotekelezwa Katika Mwaka 2015/2016 Nje ya Mpango wa BRN.....	87
9.0 SHUKRANI.....	95
10.0 .MAOMBI YA FEDHA.....	97
KIAMBATISHO NA.1.....	99
KIAMBATISHO NA.2.....	103

KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

ALAT	Muungano wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania
ATCL	Kampuni ya Ndege Tanzania
BADEA	Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi kwa Afrika
BASA	Mikataba ya Usafiri wa Anga
BRN	Programu ya Matokeo Makubwa Sasa
CATC	Chuo cha Usafiri wa Anga Dar Es Salaam
CCM	Chama cha Mapinduzi
DFID	Idara ya Serikali ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa
DMI	Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam
DRC	Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
EAC	Jumuiya ya Afrika Mashariki
HSBC	Shirika la Benki ya Hongkong na Shanghai
IBRD	Benki ya Kimataifa ya Marekebicho na Maendeleo
ICAO	Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga
ICD	Kituo cha Kupakua na Kupakia Makasha
JNIA	Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere
Km	Kilometa
LNG	Gesi asilia iliyochakatwa ili kusafirishwa
Mb	Mbunge
MCC	Shirika la Changamoto za Milenia la Marekani
Mhe	Mheshimiwa
MKUKUTA	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
MRCC	Kituo cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji Majini
MSCL	Kampuni ya Huduma za Meli
NACTE	Baraza la Vyuo vya ufundi
NIT	Chuo cha Taifa cha Usafirishaji

OFID	Mfuko wa OPEC wa Maendeleo ya Kimataifa
OPEC	Umoja wa Nchi Zinazosafirisha Petroli
RAHCO	Kampuni Miliki ya Rasilimali za Reli
Ro Ro	Meli ya Kubeba Magari
SADC	Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika
SINOTASHIP	Kampuni ya Meli ya Tanzania na China
SUMATRA	Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavuu na Majini
TAA	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania
TACAIDS	Tume ya Kudhibiti UKIMWI Nchini
TAMISEMI	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TAZARA	Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia
TCAA	Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania
TGFA	Wakala wa Ndege za Serikali
TICTS	Kitengo cha Kuhudumia Makasha Bandari ya Dar es Salaam
TIRP	Programu ya Ukarabati wa Reli ya Kati
TIRTEC	Chuo cha Reli Tabora
TMA	Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
TMEA	TradeMark East Africa
TPA	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania
TRL	Shirika la Reli Tanzania
TTFA	Wakala wa Uwezesaji wa Uchukuzi na Biashara
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
VVU	Virusi vya UKIMWI
WEF	Jukwaa la Kiuchumi Duniani
ZMA	Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar

VIONGOZI WA WIZARA



Mhe. Samuel J. Sitta (Mb)

WAZIRI



Mhe. Dkt. Charles J. Tizeba (Mb)

NAIBU WAZIRI



Dkt. Shaaban R. Mwinjaka

KATIBU MKUU



Bi. Monica L. Mwamunyange

NAIBU KATIBU MKUU

Wizara ya Uchukuzi

Dira

Kuwa Wizara inayoongoza katika ukanda wa Afrika Mashariki katika utoaji wa huduma za uchukuzi na hali ya hewa zinazokidhi viwango vya Kimataifa.

Dhima

Kuwezesha kuwa na huduma na miundombinu ya uchukuzi ambazo ni salama, zinazotegemewa, zilizo na uwiano na ambazo zinakidhi mahitaji ya usafiri na uchukuzi katika kiwango bora kwa bei nafuu na zinazoendana na mikakati ya Serikali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii zikiwa endelevu kiuchumi na kimazingira.

**HOTUBA YA WAZIRI WA UCHUKUZI, MHE.
SAMUEL J. SITTA (MB), AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA
MWAKA 2015/2016**

1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee, lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2015/2016.

2. **Mheshimiwa Spika**, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha ili tujadili utendaji wa Sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa kwa mwaka 2014/2015 na mipango ya sekta hizo kwa mwaka 2015/2016.

3. **Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 28 Februari, 2015 tulipatwa na huzuni kubwa kufuatia kifo cha ghafla cha Mheshimiwa John Damiano Komba, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi. Natoa pole kwa familia ya marehemu na wananchi wa Jimbo hilo kwa kumpoteza mpendwa wao. Aidha, natumia fursa hii kuwapa

pole wale wote waliopata maafa na hata kupoteza ndugu zao kufuatia mvua kubwa zilizonyesha katika maeneo mbalimbali nchini hususan Jijini Dar es Salaam. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahala pema peponi - Amina.

4. **Mheshimiwa Spika**, namshukuru **Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani aliyonayo kwangu kwa kunateua kuiongoza Wizara ya Uchukuzi. Nami naahidi nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa kuziongoza Wizara mbalimbali. Aidha, nawapongeza Mhe. Dkt Grace Khwaya Puja (Mb) na Mhe. Innocent Sebba (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uteuzi wao unathibitisha imani aliyonayo Mhe. Rais kwao.

5. **Mheshimiwa Spika**, niruhusu kutumia fursa hii kumpongeza **Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa amani na usalama na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 kwa umakini na umahiri mkubwa. Aidha, nampongeza **Mhe. Rais** kwa kuwa Mwenyekiti wa Nchi za Jumuiya ya Afrika

Mashariki. Nawapongeza **Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uchapakazi na uongozi wao thabiti.

6. **Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge, Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu, kwa ushirikiano mnaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu sekta ninazozisimamia za Uchukuzi na Hali ya Hewa. Nawahakikishia kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo tuliyojiwekea katika sekta zetu na Taifa kwa ujumla. Aidha, kwa namna ya pekee naomba kuishukuru familia yangu na wapiga kura wa Jimbo langu la Uchaguzi la Urambo Mashariki kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa Watanzania.

7. **Mheshimiwa Spika**, mwisho naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake **Mhe. Peter Joseph Serukamba (Mb)**, Mbunge wa Kigoma Mjini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati **Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya (Mb)**, Mbunge wa

Urambo Magharibi. Nakiri kuwa Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati katika kuchambua, kushauri na kufuatilia maendeleo ya sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa.

8. ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya kuwasilisha Hotuba hii, nawashukuru **Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu (Mb)**, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu kwa hotuba zao zilizotangulia. Hotuba hizo zimeeleza kwa ujumla maendeleo ya sekta za Kijamii na Kiuchumi kwa mwaka 2014/2015 na mwelekeo kwa mwaka 2015/2016.

9. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninatoa ufafanuzi wa kina kuhusu taarifa ya utekelezaji wa mipango na bajeti ya mwaka 2014/2015 na malengo ya mwaka 2015/2016.

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA 2014/2015

10. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mipango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 umezingatia Dira ya Maendeleo

2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016), MKUKUTA II, Mpango wa Matokeo Makubwa sasa (Big Results Now - BRN), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 pamoja na Ahadi na Maagizo ya Serikali.

11. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi katika sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa kwa kiasi kikubwa umeendelea kutegemea fedha kutoka Serikalini. Katika mwaka 2014/2015, Bunge lako Tukufu liliidhinisha bajeti ya **Shilingi bilioni 538.75**. Kati ya hizo, **Shilingi bilioni 448.63** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi bilioni 90.12** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa, **Shilingi bilioni 287.14** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 161.49** ni fedha za nje kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

12. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Mei, 2015, Wizara ya Uchukuzi ilikuwa imepokea fedha za ndani **Shilingi bilioni 86.66** sawa na asilimia **30.18** na fedha za nje **Shilingi bilioni 8.09** sawa na asilimia **5.01** kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida, Wizara ilipokea **Shilingi bilioni 89.13** sawa na asilimia **98.90** ya bajeti iliyooidhinishwa.

2.1 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MATOKEO MAKUBWA SASA (BIG RESULTS NOW – BRN) KATIKA MWAKA 2014/2015

13. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ambao ulianza mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2014/2015, miradi ya BRN iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 251.46**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **bilioni 195.46** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 56.0** ni fedha za nje. Hadi kufikia Mei, 2015, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 55.80** sawa na **asilimia 28.5** ya fedha za ndani zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya BRN.

2.1.1 Utekelezaji wa BRN Katika Sekta ya Bandari

14. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuzingatia viashiria mbalimbali, huduma za Bandari ya Dar es Salaam zimeendelea kuwa bora. Hadi kufikia Aprili, 2015, muda wa meli kukaa Bandarini kwa ajili ya kupakia au kupakua mizigo (ship turn around time) ulipungua na kufika siku 3.1 ikilinganishwa na siku 4.8 zilizofikiwa Mei, 2014. Uwezo wa Bandari kupakua magari (Roll on Roll Off capacity) kwa kila zamu moja ya saa

8 uliongezeka na kufikia magari 852 ikilinganishwa na magari 800 Mei, 2014 na idadi ya shehena zilizohudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam ilifikia tani milioni 12.7 Aprili, 2015 ikilinganishwa na tani milioni 10.3 za Mei, 2014. Aidha, muda wa kontena kukaa bandarini kabla ya kutolewa (container dwell time) ulifikia siku 9.5 Aprili, 2015 kutoka siku 9.3 Mei, 2014. Kushuka kwa ufanisi kulitokana na zoezi la uoanishaji wa mifumo ya kompyuta ya Mamlaka ya Mapato (TRA) yaani kutoka ASYCUDA++ kwenda TANCIS.

15. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuwaweka pamoja wadau muhimu wanaotoa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam (One Stop Center) ambapo huduma hii itaimarika zaidi baada ya kukamilika ujenzi wa Jengo la Bandari Agosti, 2015.

16. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato wanaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuwaunganisha pamoja watoa huduma kwa njia ya mtandao (Electronic Single Window System-eSWS). Mradi huu ulianza kujengwa Aprili, 2014 na ulitarajiwa kuanza kutumika Mei, 2015. Hata hivyo, kutokana na TRA kubadili mfumo wa kodi kutoka ASYCUDA++ kwenda TANCIS, mfumo wa eSWS

sasa inabidi ufanyiwe marekebisho ili uoane na *TANCIS*. Kazi ya kuoanisha mifumo hiyo inatarajiwa kukamilika Desemba, 2015. Lengo la mradi huu ni kuwaunganisha pamoja watoa huduma wote wa Bandari kwa njia ya mtandao ili kuongeza ufanisi.

17. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari inaendelea kutekeleza mradi wa Mfumo wa Usalama Bandarini (Integrated Security System-ISS) tangu Oktoba, 2014 unaotarajiwa kukamilika Septemba, 2015. Mradi huu utakapokamilika utaimarisha zaidi usalama wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na hivyo kuvutia wateja wengi na kuongeza mapato ya Mamlaka na Taifa kwa ujumla.

18. ***Mheshimiwa Spika***, uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya uboreshaji wa gati namba 1-7 pamoja na ujenzi wa gati la magari (RoRo) katika Bandari ya Dar es Salaam ulikamilika Mei, 2015. Taarifa ya uchambuzi wa zabuni (technical proposal) kwa ajili ya huduma ya kusimamia utekelezaji wa mradi huu iliwasilishwa Benki ya Dunia Mei, 2015 ili kupata ridhaa. Ufunguzi wa zabuni (financial proposals) kwa ajili ya tathmini ya mazingira (ESIA) ya uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam uliridhiwa na Benki ya Dunia Aprili,

2015. Mwaliko wa zabuni (Request for Proposals - RFP) kwa ajili ya kumpata Mshauri Mwelekezi wa kutengeneza andiko la biashara (business case) kwa ajili ya uendeshaji wa gati namba 5 - 7 kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya Umma na sekta binafsi (PPP) ilifunguliwa Machi, 2015 na uchambuzi unaendelea. Kukamilika kwa mradi huu kutaiwezesha Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia meli kubwa na za kisasa (Panamax ships), kupunguza msongamano na muda wa meli kusubiri kuingia bandarini na hivyo kuongeza ufanisi wa bandari.

2.1.2 Utekelezaji wa BRN Katika Sekta ya Reli

19. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu miradi ya reli, kazi ya kuhamisha baadhi ya mali za RAHCO kwenda TRL kwa lengo la kuboresha huduma za reli nchini zinaendelea vizuri. Zoezi la uchambuzi wa mali zitakazohamishwa na majadiliano baina ya wadau limekamilika. Hati (Government Notice) ya Uhamishaji wa mali kutoka RAHCO kwenda TRL ilitolewa na Serikali tarehe 22 Januari, 2015. Mali hizo ni pamoja na vichwa vya treni 79, mabehewa ya abiria 101 na mabehewa ya mizigo 1,294.

20. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia kukamilika kwa ujenzi wa madaraja mawili yaliyopo Km 293 na Km 303 kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe Aprili, 2014 na daraja moja kati ya stesheni za Bahi na Kintiku (Km 517) Septemba, 2014, Serikali kupitia RAHCO iliendelea na kazi ya kukinga madaraja hayo kwa kujenga kingo za mto ili kuzuia uharibifu unaotokana na maporomoko na mafuriko. Kazi hiyo ilikamilika Januari, 2015.

21. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, kazi ya kutandika reli zenye uzito mkubwa ili kuongeza uwezo wa reli kubeba mizigo mizito, kuhimili mwendokasi wa juu na kupunguza ajali za treni iliendelea kutekelezwa. Aidha, uchomeleaji wa maungio na uimarishaji wa reli mpya zilizotandikwa, uimarishaji wa tuta, uwekaji na ushindiliaji wa kokoto, utengenezaji wa mifereji ya maji ya mvua na uwekaji alama za reli katika eneo la Kitaraka hadi Malongwe (Km 89) umekamilika. Katika jitihada za kuendelea na utandikaji wa reli zenye uzito mkubwa, makabrasha ya kualika zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa kutandika reli ya Igalula - Tabora (Km 37) na Dar es Salaam - Munisagara (Km 52) yalikamilika Machi, 2015. Ujenzi wa miradi hii unatarajiwa kuanza Agosti, 2015 baada ya Benki ya Dunia kuidhinisha matumizi ya fedha za mkopo Machi, 30, 2015.

22. **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba ya mwaka 2014/2015, tulitoa taarifa ya Serikali kuanza kufanya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha njia ya reli kati ya Tabora na Kigoma na Kaliua - Mpanda. Kampuni ya COWI ya Denmark ilianza kazi ya upembuzi wa awali wa reli hiyo Februari, 2015 na inatarajiwa kukamilika Desemba, 2015. Aidha, Mshauri Mwelekezi, Kampuni ya HP Gauff kutoka Ujerumani alianza kazi ya usanifu wa mradi wa ujenzi wa reli ya Uvinza - Musongati na Mpanda - Karema kwa kiwango cha Kimataifa Machi, 2015 na anatarajiwa kukamilisha Januari, 2016.

23. **Mheshimiwa Spika**, kazi ya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha reli ya Isaka - Mwanza iliyoanza Septemba, 2013, ilikamilika Desemba, 2014. Aidha, Mshauri Mwelekezi anayefanya tathmini ya ulipaji fidia wa eneo la Buhongwa kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya kupanga mabehewa na kugeuzia treni (marshalling yard) anaendelea na kazi.

24. **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba ya mwaka 2014/2015, Bunge lako Tukufu liliarifiwa kuwa Serikali ipo kwenye mchakato wa kupata Mkopo wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 300 kwa ajili ya Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu na Huduma za Reli ya Kati (Tanzania Intermodal and Rail

Development Project - TIRP). Nachukua fursa hii kutoa taarifa kuwa Serikali imekamilisha maandalizi ya mradi wa ukarabati wa reli kati ya Bandari ya Dar es salaam na Isaka na Benki ya Dunia imetoa kibali cha kuanza kutumia fedha hizo tarehe 30 Machi, 2015. Mradi huu sasa utanza kutekelezwa Agosti, 2015. Kazi zitakazohusika katika utekelezaji wa mradi huu ni:

- (i) Uboreshaji wa reli kwa kufanya ukarabati mkubwa wa njia ya reli kati ya Dar es Salaam - Munisagara (Km 269) na Igalula - Tabora (Km 39); Ukarabati na uimarishaji wa madaraja mabovu na dhaifu ili yafikie uwezo wa kupitisha angalau tani 18 kwa ekseli na uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano;
- (ii) Ununuzi wa injini tatu (3), mabehewa 44 na vitendea kazi vingine;
- (iii) Uboreshaji wa vituo vya kupakua na kupakia Makasha vya Isaka, Ilala na Bandarini Dar es Salaam (Rail Platform); na
- (iv) Uimarishaji wa Taasisi na Mafunzo (Wizara ya Uchukuzi, SUMATRA, TRL na RAHCO).

25. **Mheshimiwa Spika**, maandalizi ya mkataba wa kufanya usanifu na kuanza ujenzi wa madaraja 16 kati ya 25 yaliyo katika hali mbaya (Condition E) kati ya Dar es Salaam na Tabora na mkataba wa mshauri mwelekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa kuinua uwezo wa madaraja ya reli ili kufikia tani 25 kwa ekseli yamekamilika Mei, 2015. Ujenzi wa madaraja matatu (3) na usanifu wa daraja moja (1) kati ya haya umekamilika. Kazi zilizobaki zitaanza kutekelezwa Juni, 2015.

26. **Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na tatizo la kujaa mchanga kwenye makalavati yaliyopo kati ya stesheni za Gulwe na Godegode kila mara mvua inaponyesha, Wizara ilikamilisha kazi ya kufanya usanifu wa awali wa ujenzi wa daraja (Km 349/5c) kati ya stesheni za Godegode na Gulwe Desemba, 2014. Kazi ya usanifu wa kina wa ujenzi wa daraja hilo inaendelea. Ujenzi wa daraja hilo pia utahusu kutengeneza mkondo wa maji (river training) na usimamizi wake. Daraja hili litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kubeba tani 25 kwa ekseli.

27. **Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kuwa tatizo hilo linapata ufumbuzi wa kudumu, Wizara kupitia RAHCO imepata msaada kutoka Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la JICA wa kufanya upembuzi yakinifu wa kutafuta

ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la uharibifu wa miundombinu ya reli kati ya stesheni hizo linalojirudia kila msimu wa mvua kubwa. Kazi hiyo ilianza Novemba, 2014 na inatarajiwa kukamilika Februari, 2016. Wataalam hao wameainisha maeneo hatarishi na mahitaji ya Shilingi bilioni 3.3 ili kuyaboresha.

28. **Mheshimiwa Spika**, kazi ya kuandaa Mkataba wa Mshauri Mwelekezi atakayefanya kazi ya usanifu wa kina wa ujenzi wa mabwawa mawili makubwa ya kupunguza kasi ya maji maarufu kama “punguza” ya Kimagai na Msagali imekamilika. Usanifu na ujenzi wa mabwawa hayo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2015/2016.

29. **Mheshimiwa Spika**, uboreshaji wa huduma za reli umeanza kuonesha mafanikio baada ya vifaa mbalimbali kuwasili nchini. Vifaa na mitambo iliyopatikana ni pamoja na:

- (i) Vichwa vipya vya treni 7 kati ya vichwa 13 vilivyoagizwa vimewasili hadi Mei, 2015. Vichwa vipya 6 vilivyobaki vinategemewa kuwasili Juni, 2015;
- (ii) Mabehewa mapya 22 ya abiria yaliwasili nchini Desemba, 2014. Mabehewa haya yalianza kutoa

huduma ya treni maalum (Deluxe) kuelekea mikoa ya Kigoma na Mwanza tarehe 01 Aprili, 2015;

- (iii) Mabehewa 197 kati ya 274 ya mizigo yameshawasili nchini hadi Aprili, 2015. Mabehewa 77 yaliyobaki yanategemewa kuwasili Juni, 2015. Kazi ya kukagua ubora wa mabehewa hayo inaendelea;
- (iv) Mabehewa 17 kati ya 34 ya breki yaliwasili nchini Januari, 2015. Mabehewa 17 yaliyobaki yanategemewa kuwasili Juni, 2015;
- (v) Mtambo wa kunyanyulia mabehewa uliwasili nchini Machi, 2015;
- (vi) Mabehewa 25 ya kubebea kokoto yaliwasili nchini Julai, 2014 na yanaendelea kufanyiwa majaribio kabla ya kukabidhiwa rasmi kwa TRL;
- (vii) Awamu ya kwanza ya uundaji upya wa vichwa vinane (8) vya treni ilikamilika Oktoba, 2014 katika karakana ya reli Morogoro. Vichwa hivi vinaendelea kufanya kazi kwa ufanisi;

- (viii) Awamu ya pili ya uundaji wa vichwa vingine vinane (8) vya treni inaendelea, kichwa 1 kimekamilika na kingine kitakamilika Juni, 2015;
- (ix) Ukarabati wa mabehewa 89 ya mizigo na mabehewa 31 ya abiria umekamilika;

30. **Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa vifaa hivyo umeongeza uwezo wa TRL kusafirisha mizigo kutoka tani 12,000 hadi tani 24,000 kwa mwezi, hii ni sawa na kubeba mizigo ambayo ingebebwa na malori 800 kwa mwezi; safari za treni ya abiria zimeongezeka kutoka 2 hadi 3 kwa wiki; muda wa safari umepungua kutoka siku 3 mpaka siku 2 kutokana na ubora wa vichwa na gharama za usafirishaji kupungua.

31. **Mheshimiwa Spika**, tarehe 25 - 26 Machi, 2015, ulifanyika Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Ukanda wa Kati (Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi na DRC) Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulikuwa na lengo la kukubaliana miradi ya kipaumbele katika Ukanda wa Kati na kuiuza kwa wawekezaji chini ya mwamvuli wa Jukwaa la Uchumi Duniani (World Economic Forum - WEF). Aidha, wakati wa mkutano huo, Marais wa Nchi Wanachama

wa Ukanda wa Kati kwa kushirikiana na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walizindua huduma za treni maalum (block trains) kwenda nchi za Uganda, DRC, Burundi na Rwanda.

2.2 HUDUMA ZA UCHUKUZI KWA NJIA YA NCHI KAVU

2.2.1 Usafiri na Uchukuzi kwa Njia ya Barabara

32. **Mheshimiwa Spika**, mchango wa sekta binafsi katika ukuaji wa sekta ya usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara umeendelea kuongezeka. Katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, Wizara kupitia SUMATRA ilitoa leseni za usafirishaji 33,415 kwa magari ya mizigo ikilinganishwa na leseni 28,896 zilizotolewa kipindi kama hicho mwaka 2013/2014. Ongezeko hilo la leseni ni sawa na asilimia 15.6. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, leseni za usafirishaji 22,810 zilitolewa kwa magari ya abiria ikilinganishwa na leseni za usafirishaji 21,406 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2013/2014. Ongezeko hilo la leseni ni sawa na asilimia 6.6.

33. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali imekabiliwa na ama migomo au tishio la migomo kutoka kwa madereva na wamiliki wa magari kwa nyakati tofauti kutokana na sababu mbalimbali. Baada ya Serikali kutafakari hali hii, tarehe 2 Mei, 2015, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda Kamati ya Kudumu ya kusimamia usafiri wa barabarani nchini. Lengo la Kamati hiyo ni kuhakikisha kwamba wakati wote bila kusubiri migomo, kuwe na majadiliano shirikishi ya wadau wote ili kuyapatia ufumbuzi matatizo ya makundi mbalimbali katika usafiri wa barabarani. Kamati hiyo inahusisha wadau wote muhimu wakiwemo madereva, wamiliki wa magari ya abiria na mizigo, Wizara za Uchukuzi, Mambo ya Ndani ya Nchi, Ujenzi, Kazi na Ajira na Fedha. Kamati hiyo imeshafanya vikao viwili. Kikao cha kwanza kilifanyika tarehe 12 Mei, 2015 na cha pili kilifanyika tarehe 21 Mei, 2015.

34. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Bunge lako tukufu, natoa wito kwa wadau wote wa usafiri wa barabara hususan viongozi wa madereva na wamiliki wa vyombo vya usafiri (TABOA na TATO) kushiriki kikamilifu katika vikao vya Kamati hii ili kujadili na kupata ufumbuzi wa madai yao.

35. **Mheshimiwa Spika**, hivi sasa barabara ndio njia kuu ya usafiri nchini inayotegemewa

na wananchi wa mijini na vijijini kwa ajili ya kusafirisha mizigo yao na wao wenyewe. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, njia hii ya usafiri imeendelea kukabiliwa na changamoto ya usalama barabarani. Wizara kupitia SUMATRA, imeendelea kutumia msembo wa *Paza sauti, timiza malengo yako* ili kuwahamasisha watumiaji wa usafiri wa barabara kutoa taarifa pale wanapohisi dalili zinazotishia usalama wao na mali zao. Ili kutoa taarifa hizo kwa urahisi, SUMATRA imeanza kutumia namba za simu zisizolipiwa tozo na mtumiaji anayetoa taarifa yoyote inayohatarisha usalama barabarani. Namba hizo ni 0800110019 na 0800110020. Naendelea kuwasihia wananchi kutumia namba hizo kutoa taarifa, nasi tutachukua hatua stahiki mara moja.

2.3.2 Huduma za Usafiri na Uchukuzi Mikoani na Vijijini

36. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hususan Wizara ya Ujenzi; Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na sekta binafsi inaendelea kuboresha miundombinu na huduma za uchukuzi kwa njia ya barabara nchini katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji. Kuendelea kuimarika kwa hali za barabara kumeongeza ushindani katika

utoaji wa huduma za usafiri wa magari ya abiria na mizigo. Udhibiti wa nauli za kikomo unaofanywa na SUMATRA pamoja na uboreshaji wa huduma za usafiri wa barabara mikoani na vijijini umechangia kudhibiti upandaji holela wa nauli.

2.3.3 Huduma za Usafiri Mijini

37. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kusisitiza umuhimu wa ushiriki wa sekta binafsi katika kuboresha miundombinu na kutoa huduma za usafiri wa abiria katika miji na majiji. Tunaishukuru sekta binafsi kuendelea kujitokeza katika utoaji wa huduma za usafiri wa abiria kwa njia ya barabara. Lengo la Serikali ni kuishawishi sekta binafsi ili ishiriki katika ujenzi wa miundombinu na utoaji wa huduma za usafiri wa abiria katika miji na majiji kwa njia nyingine ikiwemo maji na reli. Hii itasaidia kupunguza msongamano wa magari barabarani ambao tumekuwa tukikabiliana nao katika miji na majiji hususan Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na Mwanza.

2.3.4 Huduma za Usafiri wa Reli Jijini Dar es Salaam

38. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kupunguza

msongamano wa magari barabarani katika Majiji na Miji yetu hususan Jiji la Dar es Salaam. Moja ya hatua zilizochukuliwa ni kuboresha na kuimarisha usafiri wa treni ya abiria katika Jiji la Dar es Salaam kutoka Stesheni ya Dar es Salaam hadi Ubungo Maziwa kwa kutumia Kampuni ya Reli (TRL) na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) kutoa huduma kama hizo kuanzia Kurasini hadi Mwakanga.

39. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, jumla ya abiria 1,186,148 walisafirishwa na TRL ikilinganishwa na abiria 1,343,763 waliosafirishwa katika 2013/2014. Hii ikiwa ni pungufu kwa asilimia 13.29. Kuhusu TAZARA, katika mwaka 2014/2015' abiria 1,255,780 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 1,460,506 waliosafirishwa katika mwaka 2013/3014. Uchakavu wa vichwa vya treni na mabehewa ndiyo sababu kubwa ya kushuka kwa idadi ya abiria waliosafirishwa.

40. Aidha, Machi, 2015 Wizara kupitia RAHCO, ilimwajiri Mshauri Mwelekezi (Kampuni ya GIBB) kutoka Afrika Kusini kufanya kazi ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli Jijini Dar es Salaam kwenda maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Kerege. Kazi hiyo ya upembuzi yakinifu itakamilika Desemba, 2015.

2.3 Usafiri na Uchukuzi kwa Njia ya Reli

41. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha na kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri wa reli nchini ili kupunguza gharama za usafirishaji na kuongeza tija. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imeendelea kuboresha mtandao wa reli uliopo na kufanya utafiti kwa ajili ya kupanua mtandao huo na kujenga reli mpya katika kiwango cha Kimataifa. Aidha, Serikali imeendelea kushughulikia upatikanaji wa mabehewa na vichwa vya treni vyenye uhakika ili kuongeza uwezo wa TRL kusafirisha mizigo na abiria. Huduma za uchukuzi wa reli zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) pamoja na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO) imeendelea na uboreshaji, uimarishaji na uandaaji wa ujenzi wa njia mpya za reli kwenda kwenye maeneo ya kimkakati.

42. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, kazi ya kufanya matengenezo ya njia ya reli kati ya Kaliua na Mpanda inaendelea. Aidha, Mshauri Mwelekezi Kampuni ya *H.P.Gauff* kutoka Ujerumani alianza kazi ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli mpya ya kutoka Mpanda hadi Karema (Km 150) kwa

kiwango cha Kimataifa Machi, 2015. Kazi hii inategemewa kukamilika Desemba, 2015. Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza ufanisi na ubora wa huduma za reli katika ukanda wa Kati hususan kuelekea nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi.

43. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, RAHCO imeendelea na maandalizi ya kuboresha reli ya Tanga (Mwambani) – Arusha na ujenzi wa reli mpya ya Arusha – Musoma kwa kiwango cha Kimataifa (standard gauge). Mshauri Mwelekezi (Kampuni ya COWI) kutoka Denmark anaendelea na kazi ya kufanya usanifu wa kuinua kiwango cha reli ya Tanga - Arusha (Km 438) kuwa katika kiwango cha Kimataifa. Kazi hii iliyoanza Septemba, 2013, ilitarajiwa kukamilika Desemba, 2014. Hata hivyo, Mshauri Mwelekezi huyo aliongezewa kazi ya kufanya usanifu wa reli ya kuunganisha uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Kazi hiyo sasa inatarajiwa kukamilika Juni, 2015.

44. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Reli ya Arusha – Musoma (km 600), kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali ya ujenzi wa reli hiyo kwa kiwango cha kimataifa iliendelea na Mshauri Mwelekezi (H.P.Gauff Ingenieure Consultant) ya Ujerumani. Kazi hii ilianza Septemba, 2013 na ilitegemewa kukamilika

Desemba, 2014. Hata hivyo, Mshauri Mwelekezi huyo aliongezewa kazi ya usanifu wa reli ya kuunganisha na njia ya reli ya Mwanza pamoja na matawi ya kuelekea Engaruka, Minjingu na Dutwa. Hivyo, kazi hii sasa inatarajiwa kukamilika Agosti, 2015. Tafiti hizi ni hatua muhimu katika kuelekea kwenye ujenzi wa reli hizo.

45. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa reli ya Dar es salaam – Isaka – Keza - Kigali (Km 1,464) na Keza – Musongati (Km 197) kwa kiwango cha Kimataifa unaendelea kutekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali za Tanzania, Rwanda na Burundi. Aidha, Mtaalam Mshauri (Transaction Advisor) atakayekuwa na jukumu la kuandaa andiko la kuuza mradi (packaging for bankability) na nyaraka za zabuni kwa mfumo wa ubia kati ya sekta ya Umma na Sekta binafsi (PPP) alianza kazi Septemba, 2014 na atakamilisha Desemba, 2015.

46. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada zinazoendelea baina ya nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda katika ujenzi wa reli ya Dar es salaam – Isaka – Keza – Kigali/Musongati kwa kiwango cha Kimataifa, na kwa kuzingatia kuwa sehemu kubwa ya reli hiyo iko upande wa Tanzania, Machi, 2015 RAHCO ilimwajiri Mtaalam Mshauri (Transaction Advisor), Kampuni ya *Rothschild* kwa ajili ya kuandaa

mradi huo kwa upande wa Tanzania. Kampuni hiyo ya *Rothschild* inamiliki mtandao wa mabengi duniani hivyo, kuikabidhi jukumu la kuandaa mradi huo ni fursa kwetu kwa mradi huo kuweza kuvutia mtandao huo wa mabengi yake kutoa fedha za ujenzi wa reli hiyo zinazokadiriwa kuwa Dola za Kimarekani Bilioni 7.6.

47. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuanzia Kampuni ya *Rothschild* imetuwezesha kupata muungano wa kampuni za ujenzi wa reli kutoka China, chini ya Kampuni ya *China Railway Materials* (CRM) itakayotusaidia kujenga reli hiyo. Makubaliano ya awali kati ya muungano huo wa kampuni na RAHCO, yamefikiwa ambapo muungano wa kampuni hizo zitatoa asilimia 10 ya gharama ya ujenzi wa reli hiyo wakati Kampuni ya *Rothschild* ikikamilisha taratibu za kuandaa mradi uweze kupata fedha kutoka kwenye mabengi. Lengo ni kuhakikisha ujenzi wa reli hiyo unaanza mwishoni mwa Juni, 2015.

48. **Mheshimiwa Spika**, kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Mtwara – Songea – Mbamba Bay na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga (Km 1000) kwa kiwango cha Kimataifa ilianza Julai, 2014 na inatarajiwa kukamilika Julai, 2015. Aidha, Makubaliano ya awali

(*Framework Contract*) ya ujenzi wa reli hii na matawi yake yalitiwa saini na Mwekezaji kampuni ya *China Railway No. 2 Engineering Group Co Ltd* Septemba, 2014.

49. **Mheshimiwa Spika**, utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam pamoja na huduma za meli katika Maziwa ya *Victoria* na Tanganyika kwa kiasi kikubwa unategemea ubora na ufanisi wa reli ya Kati. Kwa kutambua umuhimu wa reli ya Kati, Mamlaka ya Bandari Tanzania imekubaliana na TRL kuunda upya vichwa 5 vya treni kwa ajili ya kuanzisha treni maalum (block trains) kwenda Kigoma ili kuhudumia wafanyabiashara wa Kigoma, DR Congo, Burundi; na kwenda Mwanza kwa ajili ya wafanyabiashara wa maeneo ya Mwanza, Uganda na Rwanda. Mapendekezo ya utaratibu wa kukopeshana baina ya taasisi hizo yamewasilishwa Serikalini kwa maamuzi. Serikali inaendelea kupitia utaratibu huo.

50. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na tatizo la uhaba wa mtaji wa kuendeleza Kampuni na ufinyu wa bajeti kutoka Serikalini, TRL imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kuwa inatoa huduma bora. Jitihada hizo ni pamoja na kutafuta mbia mahiri na mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi za fedha. Agosti, 2014, TRL ilitiliana saini na Benki ya Rasilimali ya Tanzania (TIB)

itakayoshirikiana na benki ya Maendeleo ya Africa Kusini (DBSA) kwa ajili ya kupata mkopo wenye masharti nafuu. Benki hizo zinatatarajia kutoa mkopo wa shilingi bilioni 213.2 kwa ajili ya kuunda upya vichwa vya treni 9; kununua vichwa vya treni vipya 19 na mabehewa ya mizigo mapya 260; kuunda upya vichwa 18 vya sogeza na mtaji wa kuendeshea Kampuni. TIB imemwajiri Meneja (Collateral Manager) kwa ajili ya kusimamia mkopo huo. Aidha, TRL inaendelea kufanya matengenezo ya matenki ya mafuta yaliyo katika stesheni za Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro na Tabora kwa ajili ya kuhifadhi mafuta ambayo ni sehemu ya mkopo.

51. **Mheshimiwa Spika**, Serikali za Tanzania na Zambia zimeendelea na juhudi za uendelezaji wa miundombinu na uboreshaji wa huduma za TAZARA. Aidha, Serikali ilikamilisha utekelezaji wa miradi iliyoainishwa katika Itifaki ya 14 ya ushirikiano wa kiuchumi na kiufundi kati ya Serikali za Tanzania na Zambia kwa upande mmoja na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa upande mwingine. Miradi iliyokamilika ni pamoja na ununuaji wa vichwa vya treni vipya 6, mabehewa ya mizigo mapya 90, vipuri kwa ajili ya matengenezo ya vichwa vya treni 6; ukarabati wa vichwa vya treni vya sogeza 3; ukarabati wa mitambo ya kunyanyua mizigo 4 na ununuaji wa vipuri vya mabehewa. Kazi zilizokamilika katika utekelezaji wa itifaki

ya 15 ambayo vifaa vyake vimeanza kuwasili Septemba, 2014 ni pamoja na ununuaji wa mashine za okoa 2, mitambo na vifaa vya usalama; Vichwa vipya 4 vya treni vya sogeza ambavyo viliwasili Aprili, 2015; Vichwa vya treni vipya 4 vya njia kuu ambavyo vitawasili Julai, 2015 na mabehewa mapya 18 ya abiria ambayo yanatarajiwa kuwasili Oktoba 2015. Aidha, mtambo wa kuzalisha kokoto wa Kongolo ulifanyiwa matengenezo ili uendelee na uzalishaji wa kokoto kwa ajili ya ukarabati wa njia.

52. **Mheshimiwa Spika**, utendaji kazi wa TAZARA umekuwa ukishuka mwaka hadi mwaka kutokana na sababu kadhaa zikiwemo uchakavu wa vifaa na sheria inayoongoza uendeshaji wa Mamlaka hii. Ili kuimarisha utendaji wake, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Zambia zinaendelea na marekebisho ya Sheria iliyoianzisha TAZARA. Rasimu ya Sheria hii iliwasilishwa kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri wa TAZARA Desemba, 2014 na kutolewa maelekezo ya kufanyiwa kazi kwa pamoja na wataalam wa pande zote mbili. Kutokana na majukumu mengi kwa upande wa Zambia, ikiwemo Uchaguzi Mkuu; wataalam hao wanatarajiwa kukutana Juni, 2015. Rasimu hii itakapokamilika, itawasilishwa Serikalini kwa uamuzi kabla ya kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

53. **Mheshimiwa Spika,** mbali ya urekebishaji wa Sheria hiyo, Baraza la Mawaziri la TAZARA lilikubaliana kila nchi mwanahisa kuchangia Dola za Kimarekani milioni 40. Fedha hizi ni kwa ajili ya kufanikisha Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano (2013/2014 – 2017/2018) wa TAZARA. Hadi Aprili, 2015, Serikali imetoa Shilingi bilioni 25.9 ambapo Shilingi bilioni 11.2 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa TAZARA na Shilingi bilioni 14.7 ni kwa ajili ya mafao ya wastaafu wa TAZARA upande wa Tanzania. Aidha, Serikali itaendelea kuchangia katika uboreshaji wa TAZARA kama ilivyokubalika. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga Shilingi bilioni 44.0 kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Maendeleo wa TAZARA. Serikali ya Zambia pia imetimiza ahadi yake kwa kutenga fedha katika bajeti ya mwaka 2015.

54. **Mheshimiwa Spika,** kuhusu miradi ya kuboresha utendaji kwa kushirikiana na kampuni nyingine (Smart partnership), tayari mashirika mengine yameruhusiwa kutumia miundombinu ya reli ya TAZARA kwa kulipa tozo (access fee) au kutoa vitendea kazi kama mafuta. Wizara inaendelea kuainisha maeneo mengine yanayohitaji ushirikiano wa aina hiyo.

2.4 Udhhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini

55. **Mheshimiwa Spika,** SUMATRA imeendelea kudhibiti huduma za usafiri wa nchi kavu na majini nchini. Aidha, SUMATRA imeendelea kushirikiana na Mamlaka ya Bahari Zanzibar (Zanzibar Maritime Authority - ZMA) katika ukaguzi na uhakiki wa ubora wa vyombo vya usafiri majini, taratibu za utafutaji na uokoaji, kubadilishana taarifa muhimu zinazohusu usalama wa vyombo vya usafiri majini na uhifadhi wa mazingira ya bahari.

2.5 Udhhibiti wa Huduma za Usafiri wa Reli

56. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, SUMATRA ilifanya ukaguzi wa miundombinu ya reli na mitambo ya Kampuni za TRL na TAZARA. Ukaguzi huo ulibaini mambo kadhaa mojawapo likiwa ni kutokuwa na vizuizi katika makutano ya reli na barabara. Kufuatia ukaguzi huo, SUMATRA ilishauri Mamlaka zinazohusika kujenga matuta ya kupunguza mwendokasi wa magari kwenye makutano ya reli na barabara. Naipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kupokea ushauri huo, kwani matuta ya kusaidia kupunguza mwendokasi yamejengwa na hivyo, kupunguza

matukio ya ajali za treni katika makutano ya reli na barabara.

57. **Mheshimiwa Spika**, Agosti, 2014, SUMATRA iliendesha mafunzo ya usalama kwa wafanyakazi waliopo kwenye uendeshaji wa treni. Mafunzo hayo yalikusisha wafanyakazi 37 kutoka TRL na TAZARA. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuimarisha usalama wa usafiri wa njia ya reli nchini. SUMATRA itaendelea kutoa mafunzo ya aina hiyo kwa watoa huduma za usafiri wa barabara, reli na majini ili kuboresha huduma za uchukuzi wa nchi kavu na majini nchini.

2.6 Udhhibiti wa Huduma za Usafiri kwa Njia ya Barabara

58. **Mheshimiwa Spika**, SUMATRA pia ina jukumu la kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa kwa njia ya barabara. Katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, SUMATRA ilifanya ufuatiliaji wa ubora wa huduma ya usafiri wa abiria kwa njia ya barabara kati ya Dar es Salaam – Mbeya - Sumbawanga, Sumbawanga - Mpanda – Tabora, Tabora – Dar es Salaam na Dar es Salaam – Njombe. Katika ufuatiliaji huo, ilibainika kuwa baadhi ya mabasi yamekuwa yakitumia dereva mmoja ambaye huendesha gari kwa muda mrefu bila kuwa na mapumziko. Upungufu mwingine

ni baadhi ya mabasi kujaza abiria kupita uwezo, utozaji wa nauli zaidi ya kiwango kilichoridhiwa na hali duni ya usafi wa mabasi. Kufuatia upungufu huo, hatua stahiki kwa mujibu wa kanuni za leseni za usafirishaji zilichukuliwa dhidi ya wamiliki waliobainika kutenda makosa. Naendelea kuwasihi wamiliki wa vyombo vya usafiri wa barabara pamoja na muungano wa wasafirishaji na madereva kuzingatia kanuni na taratibu tulizojiwekea ili kuleta tija katika sekta ya Uchukuzi.

59. **Mheshimiwa Spika**, biashara ya utoaji huduma ya usafiri wa abiria kwa kutumia pikipiki za magurudumu mawili au matatu imeendelea katika maeneo ya mijini na vijijini. Ili kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Usafiri wa Pikipiki za magurudumu mawili na matatu ya mwaka 2010, SUMATRA iliingia Mikataba ya Uwakala na Halmashauri za Wilaya 160 nchini. Katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, jumla ya leseni za usafiri wa pikipiki 5,328 zilitolewa ikilinganishwa na leseni 3,842 zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2013/2014.

60. **Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha utoaji wa leseni za usafirishaji kwa pikipiki za magurudumu mawili na matatu ni wa kiwango cha chini ikilinganishwa na idadi ya pikipiki zinazotoa huduma hizo. Sababu za

uchache wa pikipiki zilizopewa leseni za usafirishaji ni pamoja na:

- (i) Mwitikio mdogo wa baadhi ya Halmashauri katika kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Usafiri wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu;
- (ii) Watumishi wa Halmashauri ambao wamepewa mafunzo kwa ajili ya kusimamia kanuni za usafiri wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu kuhama vituo vya kazi;
- (iii) Ukwepaji wa malipo ya Leseni ya Usafirishaji;
- (iv) Vijana wengi kujiingiza katika uendeshaji pikipiki bila kuwa na mafunzo na hivyo kukosa leseni za udereva; na
- (v) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya shughuli za utoaji elimu na uhamasishaji umma.

61. **Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha utekelezaji wa mikataba iliyoingiwa na Halmashauri, SUMATRA imekuwa na mawasiliano ya karibu na Halmashauri hizo. Aidha, SUMATRA imeendelea kuzikumbusha Halmashauri umuhimu wa kutekeleza mikataba hiyo kupitia mikutano ya Halmashauri nchini

inayoandaliwa na ALAT. Aidha, Aprili, 2015 SUMATRA ilitoa mafunzo kwa watumishi wote wa Halmashauri walioteuliwa kusimamia huduma za pikipiki katika maeneo yao. Ni matarajio ya Wizara kuwa utekelezaji wa makubaliano baina ya SUMATRA na Halmashauri za Wilaya utapunguza changamoto zitokanazo na usafiri wa abiria kwa kutumia pikipiki ikiwa ni pamoja na kupunguza ajali na uhalifu unaohusisha matumizi ya pikipiki hizo.

2.7 Udhhibiti wa Usalama wa Vyombo vya Usafiri Majini

62. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kuhakikisha kuwa vyombo vya usafiri majini vinakidhi viwango vya ubora unaotakiwa. Katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, SUMATRA ilikagua vyombo vikubwa na vidogo katika mikoa ya Dar es Salaam, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Mara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Tanga na Pwani. Vyombo vidogo 2,340 vilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora. Vyombo vilivyobainika kuwa na upungufu wa ubora na usalama vilielekezwa kufanyiwa marekebisho kabla ya kupewa vyeti vya ubora (Seaworthiness Certificates). Aidha, ukaguzi huo pia ulihusisha meli ya MV.Victoria inayotoa huduma kati ya Mwanza na Bukoba. Kufuatia ukaguzi huo

SUMATRA ililazimika kusimamisha huduma za meli hiyo tarehe 19 Desemba, 2014 ili ifanyiwe matengenezo makubwa.

63. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kuimarisha usimamizi wa usalama katika usafiri wa majini. Kituo cha kuratibu taarifa za Utafutaji na Uokoaji Majini (MRCC) kilichopo Dar es Salaam kimeendelea kutoa taarifa na kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji majini. Katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, idadi ya ajali za majini zilizoripotiwa katika Kituo cha MRCC kwa upande wa Tanzania Bara zilikuwa 9. Katika ajali hizo, jumla ya watu 148 waliokolewa na 35 kupoteza maisha ikilinganishwa na ajali 13 za kipindi kama hicho mwaka 2013/2014 ambapo watu 125 waliokolewa na wengine 24 kupoteza maisha.

3.0 USAFIRI NA UCHUKUZI MAJINI

3.1 Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa

64. **Mheshimiwa Spika**, licha ya wamiliki binafsi wa vyombo vya uchukuzi majini kuendelea kushiriki katika utoaji wa huduma za usafiri majini kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) pia imeendelea kutoa huduma hizo katika maziwa makuu. Kampuni hii ilisafirisha

abiria 178,812 ikilinganishwa na abiria 254,472 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2013/2014. Hii ni pungufu kwa asilimia 30. Sababu za upungufu huo ni pamoja na kusimama kwa meli ya MV. Victoria na MV. Liemba kutoa huduma. Kampuni imekamilisha matengenezo ya meli ya MV.Serengeti ili iweze kutoa huduma za uchukuzi kati ya miji ya Mwanza na Bukoba katika kipindi ambapo meli ya MV.Victoria inaendelea kufanyiwa matengenezo.

65. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu usafirishaji wa mizigo, kati ya Julai, 2014 na Aprili, 2015, Kampuni ilisafirisha tani 34,242 za mizigo ikilinganishwa na tani 50,841 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2013/2014. Hii ni pungufu kwa asilimia 33. Sababu zilizochangia kushuka kwa usafirishaji wa mizigo ni pamoja na kupungua kwa shehena inayoelekea nchini Uganda na kusimama kwa Meli ya MV. Serengeti na MV. Victoria kwa ajili ya matengenezo.

66. **Mheshimiwa Spika**, wakati bajeti ya mwaka 2014/2015 inawasilishwa, Wizara ilitoa taarifa kuhusu uchelewaji wa kuanza kwa ujenzi wa meli mpya nne katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kutokana na gharama zake kupanda kwa asilimia 163 ya gharama zilizokadiriwa awali. Mradi huu utakaogharimu

Dola za Marekani milioni 74.9, unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Denmark. Ili kurahisisha utekelezaji, mradi huu sasa umegawanywa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa meli hizo itahusisha usanifu wa kina na ujenzi wa meli moja (1) mpya katika Ziwa Victoria, meli moja mpya katika Ziwa Tanganyika na ukarabati wa meli ya MV.Umoja. Aidha, zabuni ya ujenzi wa meli hizo na ukarabati wa meli ya MV. Umoja zimetangazwa Aprili, 2015.

67. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua ya kuboresha na kuimarisha huduma za usafiri katika Ziwa Victoria, Wizara kupitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) iliendelea kuzifanyia matengenezo meli zinazotoa huduma katika ziwa hili ili ziendeele kusafirisha abiria na mizigo. Meli ya MV.Serengeti imefanyiwa matengenezo na ilianza kutoa huduma tarehe 24 Mei, 2015. Aidha, meli ya MV.Victoria ilianza kufanyiwa matengenezo ya awali tarehe 15 Aprili, 2015 kabla ya kuipandisha kwenye chelezo kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo makubwa yatakayoanza tarehe 15 Juni, 2015. Matengenezo ya meli hii yanatarajiwa kukamilika Oktoba, 2015.

68. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu na huduma zake ili kuchochea usafiri wa majini hususan katika

bandari za kwenye maziwa. Aidha, ili kuimarisha huduma za uchukuzi katika maziwa makuu, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliahidi kuanza ujenzi wa meli moja kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA). Kazi ya ujenzi wa meli mpya kwa ajili ya kutoa huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika Ziwa Nyasa ilianza Januari, 2015 na inatarajiwa kukamilika Desemba, 2015. Aidha, kazi ya ukarabati wa meli ya MV. Butiama ili kuwahudumia wananchi wa Visiwa vya Ukerewe inaendelea ambapo vipuri vya kuifanyia matengenezo meli hiyo vimeagizwa nje ya nchi.

69. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuitangaza meli ya MV. Liemba kama urithi wa Taifa (National Heritage), Agosti, 2014 Serikali za Tanzania na Ujerumani zilisaini makubaliano ya kuifanyia ukaguzi meli ya MV. Liemba. Ukaguzi huo uliokamilika Desemba, 2014 ulibaini kuwa meli hiyo bado ni imara kuweza kutoa huduma za uchukuzi endapo itafanyiwa ukarabati. Makubaliano hayo pia yalihusu kuifanyia ukarabati meli ya MV. Liemba ili iendelee kutoa huduma. Ukarabati huo utagharamiwa kwa pamoja ambapo Serikali ya Ujerumani itachangia asilimia 50, Serikali ya Tanzania asilimia 25 na sekta binafsi kutoka Ujerumani asilimia 25. Kazi inayoendelea sasa ni kufanya utafiti wa kubaini gharama halisi zinazohitajika kwa ajili ya ukarabati.

3.2 Huduma za Uchukuzi Baharini

70. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni inayomilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China (SINOTASHIP) imeendelea kutoa huduma zake kwa kutumia meli kubwa moja yenye uwezo wa kubeba tani 57,000 kwa wakati mmoja. Katika mwaka 2014/2015, meli hii ilifanya safari 7 kama ilivyopangwa. Jumla ya tani 350,000 zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 330,000 zilizosafirishwa katika mwaka 2013/2014. Lengo la idadi ya safari lilifikwiwa kutokana na meli kusafiri masafa mafupi na kupita katika bandari zisizokuwa na msongamano mkubwa wa meli.

3.3 Huduma za Bandari

71. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeendelea kuimarisha bandari za mwambao wa Bahari ya Hindi na zile za Maziwa Makuu kwa ufanisi ili ziweze kutoa huduma bora, kuchangia ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini.

72. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, Mamlaka kwa kutumia bandari zote nchini ilihudumia jumla

ya shehena ya tani milioni 14.10 (Bandari ya Dar es Salaam tani milioni 12.7 na bandari nyingine tani milioni 1.4) ikilinganishwa na tani milioni 12.51 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2013/2014. Hili ni ongezeko la asilimia 12.7. Shehena hiyo inajumuisha makasha yaliyohudumiwa na Kitengo cha Kuhudumia Makasha (TICTS). Katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, TICTS ilihudumia makasha 377,861 yakilinganishwa na makasha 351,556 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2013/2014. Hili ni ongezeko la makasha 26,305 ambayo ni asilimia 7.5.

73. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, shehena iliyohudumiwa kwenda na kutoka nchi jirani za Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Rwanda na Uganda ilikuwa ni tani milioni 4.37 ikilinganishwa na tani milioni 4.45 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2013/2014. Hii ni sawa na upungufu wa asilimia 1.8. Upungufu wa shehena unatokana na utendaji hafifu wa njia ya reli. Hata hivyo, kuna mategemeo ya kuongezeka kwa shehena kutokana na jitihada zinazoendelea za kuboresha miundombinu na huduma za reli, matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kuhudumia mizigo bandarini na kuwavutia wateja kutoka ndani na nje ya nchi.

Jitihada nyingine ni kufungua ofisi katika mji wa Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; kuimarisha usalama wa mizigo ya wateja na kutoa huduma za bandari kwa saa 24 kwa siku kwa juma.

74. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliahidi kuendelea kuhakikisha kuwa ujazo wa mafuta yanayoingia nchini ni sahihi kutokana na vipimo vilivyokubaliwa Kimataifa. Ili kuondokana na changamoto hiyo, Mkandarasi Kampuni ya *M/s. Woolgate Trademark Co. Ltd* alianza kazi ya kufunga mita za kupima ujazo wa mafuta (flowmeters) yanayoshushwa melini katika boya jipya la kushushia mafuta (SPM) Novemba, 2014. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Juni, 2016. Kufungwa kwa mita hizi kunatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali.

75. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka kwa kushirikiana na sekta binafsi inatarajia kuanza ujenzi wa gati Na. 13 na 14 katika Bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya kuhudumia makasha. Zabuni (Request for Proposal) zilizotolewa kwa kampuni 10 ili kuendeleza gati hizo kwa utaratibu wa Sanifu, Jenga, Endesha, Rejeshu (Design, Build, Operate and Transfer - DBOT) zitafunguliwa Aprili, 2016. Usogezwaji mbele wa tarehe ya ufunguzi wa zabuni hizo unatokana na wazabuni kuhitaji taarifa za ziada

ili waweze kuandaa zabuni zao. Hata hivyo, mradi huu umeanza upya kutokana na kasoro nyingi zilizobainika katika uandaaji wa taarifa za awali za ujenzi wa magati hayo.

76. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari inaendelea kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini mahitaji na namna bora ya kuziendeleza bandari za Mwanza, Musoma, Nansio, Bukoba na Kemondo Bay. Mshauri Mwelekezi, Kampuni ya *M/s Royal Haskoning* ya Uholanzi aliyeanza kazi ya upembuzi yakinifu wa bandari hizo Agosti, 2014 anatarajiwa kukamilisha Juni, 2015. Lengo la kuboresha bandari hizi ni kuzijengea uwezo wa kuhudumia shehena kubwa itakayosafirishwa kwa njia ya reli ya Kati. Aidha, baada ya taarifa ya upembuzi yakinifu kukamilika, Mamlaka itaandaa mpango wa kutekeleza mapendekezo ya utafiti huo.

77. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bandari ya Kigoma, kazi ya kukarabati chelezo kwa ajili ya matengenezo ya meli ilikamilika Novemba, 2014. Chelezo hiki kimetoa huduma ya ukarabati wa meli ya MV. Liemba. Aidha, kazi ya ukarabati wa kreni kubwa ya kupakia na kupakua shehena ya makasha ilikamilika Desemba, 2014. Kazi ya kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini mahitaji ya namna bora ya kuziendeleza bandari za Kigoma na Karema

inayofanywa na Mshauri Mwelekezi, *M/s Royal Haskoning* wa Uholanzi ilianza Aprili, 2015 na inatarajiwa kukamilika Februari, 2016.

78. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa Bandari ya Mbegani, Bagamoyo, Mradi huu umepata msukumo baada ya kampuni ya *China Merchant Holdings International Limited* (CMHI) kuifahamisha Serikali ya Tanzania kwamba taasisi ya *State General Reserve Fund* (SFRF) ya Serikali ya Oman imeomba kuingia ubia katika mradi huu Septemba, 2014. Makubaliano ya Awali (MoU) ya pande zinazohusika katika mradi huu yalisainiwa Oktoba, 2014. Makubaliano hayo yaliweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa mradi huu unatekelezwa. Moja ya mikakati hiyo ni kuunda Kamati ya Utatu (Tripartite Joint High Level Task Force). Kamati hii ilipewa kazi ya kusimamia maandalizi ya nyaraka muhimu za mradi zikiwemo Makubaliano ya Ushirikiano (Joint Venture Agreement) na nyaraka zinazohusu masuala ya kiufundi, kifedha, kiuchumi na kijamii. Kamati hiyo iliyoanza kazi Desemba, 2014, inafanya kazi chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, kazi ya kufanya uthamini wa mali katika eneo la bandari hiyo ilikamilika Oktoba, 2014. Taratibu za fidia zinaendelea.

79. **Mheshimiwa Spika**, zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kujenga Bandari ya

Mwambani – Tanga kwa utaratibu wa Sanifu, Jenga na Gharamia (Design, Build and Finance) ilitarajiwa kufunguliwa Januari, 2015 lakini hakuna mzabuni yeyote aliyejitokeza. Sababu kubwa ya kufanya wawekezaji kutojitokeza ni kukosekana kwa takwimu za kutosha za shehena katika Ukanda wa Maendeleo wa Kaskazini. Hivyo, Mamlaka inakamilisha taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi ili kurejea upembuzi yakinifu na usanifu wa bandari hiyo.

80. **Mheshimiwa Spika**, zabuni ya mradi wa kupanua Bandari ya Mtwara kwa kujenga gati mpya nne kwa utaratibu wa Sanifu, Jenga na Gharamia zilifunguliwa Novemba, 2014. Majadiliano na mkandarasi yalikamilika Mei, 2015. Kukamilika kwa mradi huu kutaiwezesha Bandari ya Mtwara kuhudumia shehena kubwa inayotarajiwa baada ya kuanza kwa uzalishaji wa gesi na mafuta katika mwambao wa Bahari ya Hindi, uchimbaji wa chuma na makaa ya mawe katika maeneo ya Mchuchuma, Liganga na Ngaka - Mbinga. Bandari hii pia itasaidia kuimarisha uendelezaji wa Ukanda wa Mtwara (Mtwara Development Corridor) na kuweza kuhudumia shehena za nchi jirani za Malawi, Msumbiji na Zambia.

81. **Mheshimiwa Spika**, mbali na ujenzi wa gati hizo nne katika Bandari ya Mtwara,

Kampuni ya Dangote imeonesha nia ya kujenga gati katika eneo la Kisiwa mkoani Mtwara. Majadiliano baina ya Mamlaka na Kampuni ya Dangote yanaendelea.

82. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari inaendelea kuboresha bandari ndogo za Kilwa, Lindi, Rushungi, Pangani na Nyamisati katika Bahari ya Hindi; Lushamba, Ntama na Kyamkwikwi katika Ziwa Victoria; Kagunga, Lagosa, Kalya, Kabwe na Kibirizi katika Ziwa Tanganyika; Kiwira na Ndumbi katika Ziwa Nyasa.

83. **Mheshimiwa Spika**, kazi ya kukarabati Bandari ya Lindi ilianza Mei, 2015 na itakamilika Mei, 2016. Lengo la ukarabati huu ni kukidhi mahitaji ya usafiri wa majini kwa wakazi wa Mkoa wa Lindi. Kuhusu ujenzi wa gati la Nyamisati – Rufiji, ujenzi wa gati hili unatarajiwa kuanza Julai, 2015 na kukamilika Juni, 2016. Kwa upande wa gati la Pangani, kazi ya usanifu wa ujenzi wa gati hili ilikamilika Aprili, 2015. Mkataba wa ujenzi utakaotekelezwa na Kampuni ya *M/s Alpha Logistics Ltd* kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.4 ulisainiwa Septemba, 2014. Ujenzi wa gati hili umeanza Mei, 2015 na unategemewa kukamilika Septemba, 2015.

84. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa magati ya Lushamba na Ntama katika Ziwa Victoria ulianza Desemba, 2014 na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2015. Kampuni ya *M/s Nangware Mhando Ltd* inajenga gati la Lushamba kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.12 na Kampuni ya *M/s Geman Engineering Co. Ltd* inajenga gati la Ntama kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.04.

85. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa magati ya Kabwe na Kiwira umetekelezwa kwa kutumia wataalam wa Mamlaka. Ujenzi wa gati la Kabwe katika Ziwa Tanganyika ulikamilika Aprili, 2015 na ule wa gati la Kiwira katika Ziwa Nyasa ulikamilika Machi, 2015.

86. **Mheshimiwa Spika**, kazi ya ujenzi wa gati la Kipiri katika Ziwa Tanganyika ilikamilika Septemba, 2014. Aidha, kazi ya kufanya uthamini wa eneo kwa ajili ya kujenga maegesho ya vyombo vidogovidogo vya usafiri majini katika eneo la Kibirizi imekamilika na malipo ya fidia ya Shilingi bilioni 2.3 yamefanyika.

87. **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba ya mwaka 2014/2015 ilitolewa taarifa ya Wakandarasi *M/S Cannopies* na *M/S Modspan* kushindwa kukamilisha ujenzi wa magati ya Kagunga, Lagosa, Sibwesa (Kalya) na Karema katika Ziwa Tanganyika na Kiwira katika Ziwa

Nyasa. Kuhusu ujenzi wa gati la Kagunga, Mamlaka imeingia mkataba wa ujenzi wa gati hili na Kampuni ya M/s *Kashere Enterprises Ltd* Aprili, 2015. Mradi huu utakaogharimu Shilingi bilioni 3.356 umeanza Mei, 2015 na utakamilika Juni, 2016. Kwa upande wa gati la Sibwesa na Lagosa, Mamlaka iko katika hatua za mwisho za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa gati hizo. Ujenzi wa gati hizo unatarajiwa kuanza Juni, 2015. Kuhusu gati la Karema, awali Mamlaka ilikuwa na mpango wa kujenga gati dogo kwa ajili ya abiria. Kutokana na umuhimu wa bandari hii kwa ajili ya mizigo inayoelekea nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kupitia Bandari ya Kalemie, imebainika ipo haja ya kujenga bandari kubwa kwa ajili ya mizigo na abiria. Mamlaka inaendelea na uchambuzi wa zabuni za kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari hii.

88. **Mheshimiwa Spika,** hatua zilizochukuliwa dhidi ya Kampuni za *Cannopies* na *Modspan* kwa kushindwa kutekeleza matakwa ya mkataba ni pamoja na kuzifikisha Kampuni hizo kwa Bodi ya Usajili wa Makandarasi, kudai fidia na kuzishtaki Kampuni hizo Mahakamani. Kesi zinaendelea.

89. **Mheshimiwa Spika,** zabuni ya ujenzi wa gati la Ndumbi ilitangazwa Aprili, 2015. Ili

kukamilisha ahadi iliyotolewa katika Bunge hili mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imeanza kazi ya ujenzi wa meli moja yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo. Ujenzi wa meli hii utakaogharimu Shilingi bilioni 9.1 ulianza Januari, 2015 na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2015.

4.0 USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA

4.1 Udhhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga

90. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imeendelea kuhakikisha kuwa viwanja vya ndege na huduma za usafiri wa anga nchini vinakidhi masharti na kanuni zilizowekwa. Ili kuhakikisha kuwa kanuni hizo zinazingatiwa, katika mwaka 2014/2015, viwanja vya ndege vya Kimataifa vya Julius Nyerere (JNIA), Abeid Amani Karume na Kilimanjaro (KIA) vilikaguliwa na kupata vyeti vya ubora kulingana na matakwa ya vigezo vya Kimataifa ya viwanja vya ndege. Aidha, viwanja vya ndege vya Arusha, Mwanza, Kigoma, Tabora, Bukoba, Mtwara, Tanga, Lindi na Iringa pia vilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora. Utekelezaji wa uboreshaji wa viwanja vya ndege

nchini ni mzuri kiwango cha kukidhi matakwa ya Kimataifa.

91. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, ndege 9 ziliandikishwa kwa mara ya kwanza nchini na kupewa vyeti vya ubora. Aidha, ndege 5 zilirudishwa zilikokodishwa baada ya kumalizika muda wa mikataba ya ukodishaji. Ndege ziliorudishwa zilikuwa zikimilikiwa na Kampuni za *Coastal Travellers*, *Zenith Aviation* na *Fastjet*. Pamoja na kurudishwa kwa ndege hizo, Kampuni hizo zilileta ndege nyingine ili kukidhi matakwa ya utoaji wa huduma za usafiri wa anga nchini.

92. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma za usafiri wa anga nchini ili kuvutia wawekezaji kutoka katika sekta binafsi au kwa ubia kati ya sekta ya Umma na sekta binafsi. Katika mwaka 2014/2015, Kampuni za ndege mpya 5 zilisajiliwa nchini ili kuanza kutoa huduma za usafiri wa anga. Hatua hii inafanya Kampuni za ndege zenye leseni ya kutoa huduma za usafiri wa anga nchini kuwa 49 ikilinganishwa na Kampuni 44 zilizokuwa zimesajiliwa mwaka 2013/2014.

93. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mikataba ya Usafiri wa Anga kati ya Tanzania na nchi

nyingine (Bilateral Air Services Agreements – BASA), Wizara imeendelea kufanya mazungumzo na nchi mbalimbali ili kuipitia upya mikataba iliyopo au kuingia mikataba mipya. Lengo la kupitia upya mikataba hiyo ni kuhakikisha kuwa inakidhi mahitaji ya soko na hali halisi ya maendeleo na mabadiliko ya uchumi Duniani. Katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, mikataba kati ya Tanzania na nchi za Zambia, Italia na Mauritius ilipitiwa upya. Aidha, Tanzania iliingia mikataba mipya na nchi za Luxemburg, Canada na Austria.

94. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na uingiaji wa mikataba mipya ya BASA, hadi Aprili, 2015, Tanzania ilikuwa imeingia mikataba ya BASA na nchi 54 ikilinganishwa na nchi 50 zilizokuwa na makubaliano ya BASA na Tanzania katika kipindi kama hicho mwaka 2013/2014. Kati ya mikataba hiyo, mikataba 22 ndiyo ambayo Kampuni au mashirika yake ya ndege yanatoa huduma kati ya Tanzania na nchi husika. Kwa sasa mashirika ya ndege yanayotoa huduma za usafiri wa anga kwa utaratibu wa BASA ni 27. Nchi nyingine bado ziko katika taratibu za kuanza kutekeleza mikataba hiyo. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, safari za ndege kati ya Tanzania na nchi zilizosaini makubaliano ya BASA zilikuwa 175 kwa juma. Kutokana na ukuaji wa sekta ya utalii na ongezeko la uwekezaji hususan katika

sekta za Nishati na Madini na Ujenzi wa Nyumba (Real Estates), inatarajiwa kuwa hadi Juni, 2015, safari za ndege zitakuwa 213 kwa juma.

95. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mashirika ya nchi nyingi zilizosaini mikataba ya BASA kufanya safari kuanzia katika nchi zao, Mashirika mapya ya *Fly Dubai* na *Air Seychelles* ndiyo yanatoa huduma za kimataifa kuanzia nchini mwetu. Nayapongeza mashirika haya kwa kuleta changamoto kubwa katika mashirika ya ndani yanayotoa huduma za usafiri wa anga hususan ATCL, *Precision* na *Fastjet*.

96. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga iliongezeka na kufikia abiria 3,852,413 ikilinganishwa na abiria 3,084,830 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2013/2014. Idadi hii inatarajiwa kuongezeka hadi kufikia abiria 4,894,328 ifikapo Juni, 2015. Idadi ya abiria waliosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi inategemewa kuongezeka kutoka abiria 1,945,961 mwaka 2014/2015 na kufikia abiria 1,988,772 katika mwaka 2015/2016. Hili ni ongezeko la asilimia 2.2. Aidha, idadi ya abiria wa ndani inatarajiwa kuongezeka kutoka abiria 2,948,367 katika mwaka 2014/2015 hadi kufikia abiria

3,128,218 mwaka 2015/2016. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 6.1.

97. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu safari za ndege (aircraft movements), katika mwaka 2014/2015, jumla ya safari za ndege 245,604 zilifanyika ikilinganishwa na safari 238,760 za mwaka 2013/2014. Hili likiwa ni ongezeko la asilimia 2.8. Kati ya safari hizi, safari za kimataifa ziliongezeka kutoka safari 39,910 mwaka 2013/2014 hadi kufikia safari 40,789 mwaka 2014/2015, sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Safari za humu nchini pia ziliongezeka kutoka safari 198,850 mwaka 2013/2014 hadi kufikia safari 204,815 mwaka 2014/2015, sawa na ongezeko la asilimia 3.

98. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, mizigo iliyosafirishwa kwenda na kutoka nje ya nchi ilifikia tani 30,838 ikilinganishwa na tani 29,918 zilizosafirishwa mwaka 2013/14. Hili ni ongezeko la asilimia 3. Takwimu hizi zinaonesha ukuaji wa sekta ndogo ya usafirishaji wa mizigo kwa njia ya anga.

99. **Mheshimiwa Spika**, sekta ndogo ya usafiri wa anga nchini imeonesha kuendelea kuimarika ambapo ukuaji wake kwa kiasi kikubwa umechangiwa na ukuaji wa uchumi wa ndani na nje ya nchi. Sababu nyingine zilizochangia katika ukuaji huo ni pamoja na

kuongezeka kwa utalii nchini; kuongezeka kwa safari za ndege katika kiwanja cha ndege cha Songwe na kukarabatiwa kwa viwanja vya ndege. Aidha, kusainiwa kwa mikataba ya BASA kati ya Tanzania na nchi nyingine; mashirika ya ndege ya *Emirates*, *Royal Dutch Airline (KLM)* na *Qatar Airways* kuongeza safari zao za ndege na mashirika mapya ya ndege kuanza kutoa huduma za usafiri wa anga kimataifa pia zimechangia katika ukuaji wa utoaji wa huduma za usafiri wa anga nchini.

100. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TCAA imeendelea kuhakikisha kuwa matukio na ajali katika usafiri wa anga zinapungua. Katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, matukio 4 na ajali 2 za ndege zilitokea. Ajali hizi zilisababisha vifo vya watu 4 na ndege zote kuharibika kabisa. Uchunguzi wa vyanzo vya ajali zote mbili bado unaendelea.

101. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Usafiri wa Anga kwa sasa inaendelea na matayarisho ya ukaguzi wa usalama wa anga (ICAO Universal Security Audit Programme-USAP) ambao umepangwa kufanyika Septemba, 2015. Aidha, upungufu uliobainika katika ukaguzi wa Septemba, 2014 kwenye viwanja vya ndege vya JNIA na Abeid Aman Karume unaendelea kufanyiwa kazi.

102. **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba ya mwaka 2014/2015, Serikali iliahidi kuanza kushughulikia suala la kutenganisha majukumu ya udhibiti wa usafiri wa anga na utoaji huduma ya uongozaji wa ndege. Napenda kutoa taarifa kuwa, Mtaalam Mwelekezi atakayefanya kazi ya uchambuzi yakinifu wa utenganishaji wa majukumu hayo mawili anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo Juni, 2015.

103. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara ilipanga kununua rada mpya 2 za kuongozea ndege za kiraia. Taratibu za ununuzi wa rada hizo zinaendelea ambapo nyaraka za aina ya rada hizo (specifications) zimewasilishwa ICAO kwa ajili ya kuidhinishwa. Kufungwa kwa rada hizi mpya kutaendelea kulifanya anga la Tanzania kuwa salama zaidi.

104. **Mheshimiwa Spika**, mpango wa kubadilisha mfumo wa mawasiliano ya anga kutoka mfumo unaotumika sasa wa kutumia vituo katika viwanja vya ndege kwenda mfumo wa mawasiliano wa dijitali unaofuatilia safari za ndege unaendelea kutekelezwa. Kazi ya kubadilisha mfumo huo katika viwanja vya ndege vya Dar es Salaam, Zanzibar, Kilimanjaro, Songwe, Mwanza, Tanga, Tabora, Iringa na Arusha imekamilika. Kazi ya kubadilisha mfumo katika viwanja vya ndege vya Mtwara, Songea na Kigoma inatarajiwa

kukamilika Juni, 2015. Mfumo huu mpya utapunguza gharama za mawasiliano na kuleta uhakika wa mawasiliano baina ya vituo vya kuongozea ndege.

105. **Mheshimiwa Spika**, kazi ya kufunga mtambo wa kuboresha mawasiliano kati ya waongoza ndege na marubani wakiwa angani (VHF area cover relay station) katika kituo cha Mnyusi, Tanga imekamilika kama ilivyoahidiwa katika Hotuba ya mwaka 2014/2015.

106. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliahidi kuendelea kulifanya anga la Tanzania kuwa salama katika usafiri wa anga. Napenda kulieleza Bunge hili kuwa, mradi wa kufunga mitambo ya ufuatiliaji wa mwenendo wa ndege angani (Automatic Dependence Surveillance – Broadcast - ADS-B) unaendelea vizuri. Mitambo hii husaidia ufuatiliaji wa mienendo ya ndege angani na hivyo kutoa fursa ya kuongoza ndege kwa uhakika na salama katika anga husika. Awamu ya kwanza ya ufungaji wa mitambo hii itakayohusu upande wa Mashariki hadi juu ya bahari ya Hindi inatarajiwa kukamilika Juni, 2015.

107. **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba ya mwaka 2014/2015, ilitolewa taarifa kuwa Mfuko wa Mafunzo ya Marubani na Wahandisi wa

Ndege ulianza kutumika kwa kufadhili wanafunzi 5 katika mafunzo ya urubani. Napenda kulieleza Bunge hili kuwa utekelezaji wa malengo ya Mfuko huu unaendelea vizuri. Aidha, wanafunzi 4 kati ya 5 walioenda mafunzoni wamehitimu mafunzo yao. Kampuni ya ndege ya *Precision Air* iliwaajiri vijana hao na kuwapeleka kwenye mafunzo zaidi ya aina ya ndege wanazotumia (type rating). Lengo la Mfuko huu ni kuziba pengo la uhaba wa marubani na wahandisi wa ndege unaoikabili nchi.

4.2 Huduma za Viwanja vya Ndege

108. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iliendelea na majukumu yake ya kuhudumia na kuboresha miundombinu na huduma za viwanja vya ndege nchini. Viwanja hivyo vimeendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali ili kuwezesha ndege kutua na kuruka kwa usalama. Aidha, viwanja hivyo vilifanyiwa ukarabati wa miundombinu na uboreshaji wa mitambo.

109. **Mheshimiwa Spika**, awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la Tatu la Abiria (Terminal III Building) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) inaendelea vizuri. Kazi zinazoendelea ni ufungaji wa vyuma

vya paa na ujenzi wa maegesho ya ndege na magari. Kazi za ujenzi wa jengo hili zinatarajiwa kukamilika Mei, 2016. Wizara inaendelea kutafuta fedha ili kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo hilo. Kukamilika kwa awamu zote mbili kutawezesha jengo hili kuhudumia abiria milioni 6 kwa mwaka.

110. **Mheshimiwa Spika**, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kimeendelea kuboreshwa ili kuchangia katika ukuaji wa biashara za maua, mbogamboga, matunda na utalii. Katika mwaka 2014/2015, kazi za ukarabati na upanuzi wa kiwanja hiki ili kiweze kuhudumia ndege 20 kutoka 10 za sasa kwa saa ziliendelea. Mkataba wa kuanza kazi za ukarabati na upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, barabara za viungio, jengo la abiria, ujenzi wa barabara mpya ya kiungio, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ujenzi wa mfumo mpya wa maji taka ulisainiwa Machi, 2015. Kazi za ukarabati zinatarajiwa kuanza Juni, 2015.

111. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea na kazi za kuboresha kiwanja cha ndege cha Mwanza. Kazi zilizotekelezwa katika mwaka 2014/2015 ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa jengo la kuongozea ndege (control tower) ambapo ujenzi umefikia hatua ya *control cabin*;

ujenzi wa jengo la mizigo umefikia hatua ya *super structure* na uwekaji wa tabaka la kwanza la lami katika barabara inayorefushwa ya kuruka na kutua ndege. Kazi zingine zinazoendelea ni ujenzi wa tabaka la mwisho la lami kwenye maegesho ya ndege za abiria na maegesho ya ndege za mizigo na Viungio vyake.

112. **Mheshimiwa Spika**, katika hotuba ya mwaka 2014/2015 tuliahidi kukamilisha ujenzi wa maegesho ya ndege na jengo la abiria katika kiwanja cha ndege cha Songwe. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha maegesho ya ndege; kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria pamoja na barabara ya kuunganisha (by pass road) kijiji cha Iweleje na barabara kuu ya Mbeya – Tunduma; ununuzi wa gari la pili la zimamoto; usimikaji wa kamera za usalama (CCTV) na ununuzi wa mitambo maalum kwa ajili ya huduma kwa abiria na mizigo.

113. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea na kazi ya kukarabati kiwanja cha ndege cha Bukoba kwa kiwango cha lami. Katika mwaka 2014/2015, kazi za ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari kwa kiwango cha lami zilikamilika. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa jengo jipya la abiria, ufungaji mifumo ya maji safi na taka, ufungaji

umeme, usimikaji wa kaunta za kisasa za kuhudumia abiria na uwekaji wa mikanda ya kusogezea mizigo. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Juni, 2015.

114. **Mheshimiwa Spika**, maandalizi ya utekelezaji wa awamu ya pili ya kazi za ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Kigoma na Tabora kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) yaliendelea na zabuni zinatarajiwa kutangazwa Julai, 2015. Aidha, taarifa za uchambuzi wa zabuni za kazi za ukarabati wa maegesho ya ndege na ujenzi wa uzio wa usalama wa viwanja hivyo zimewasilishwa Benki ya Dunia ili kupata ridhaa (No Objection). Kazi za awamu ya pili zitahusisha ukarabati wa barabara ya pili ya kutua na kuruka ndege, barabara ya kiungio na maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami; ujenzi wa uzio wa usalama; usimikaji wa taa (AGL) na mitambo ya kuongozea ndege aina ya DME na VOR.

115. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, TAA ilipanga kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria, maegesho ya magari, ukarabati wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani pamoja na kituo cha umeme katika kiwanja cha ndege cha Mafia. Kazi hizo hazikuweza kutekelezwa kutokana na uhaba wa fedha.

116. **Mheshimiwa Spika**, kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege kumi na moja (11) vya Lake Manyara, Musoma, Iringa, Tanga, Songea, Kilwa Masoko, Lindi, Moshi, Njombe, Simiyu na Singida kwa kiwango cha lami inaendelea na itakamilika Juni, 2015. Hatua hii itawezesha kuendelea na majadiliano na Taasisi za kifedha kwa ajili ya kuanza ujenzi na upanuzi wa viwanja hivyo.

117. **Mheshimiwa Spika**, zabuni kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga na Sumbawanga chini ya ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya yamekamilika na kuwasilishwa Benki ili kupata ridhaa. Zabuni hizi zinatarajiwa kutangazwa Julai, 2015 na kazi za ukarabati na upanuzi kuanza Oktoba, 2015. Kazi zitakazofanyika katika viwanja hivyo ni upanuzi wa barabara za kuruka na kutua ndege, barabara za viungio na maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami; ujenzi wa majengo ya abiria, maegesho ya magari; barabara za kuingia viwanjani na usimikaji wa taa (AGL) na mitambo ya kuongozea ndege aina ya DME na VOR.

118. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, kazi za kufanya matengenezo ya kawaida ili kuruhusu ndege kuruka na kutua

kwa usalama katika kiwanja cha ndege cha Mtwara ziliendelea kutekelezwa. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuboresha na kupanua kiwanja hiki kwa kiwango cha lami. Aidha, Wizara inaendelea kufanya mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ili kupata fedha za kugharamia usanifu wa kina wa miundombinu na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Msalato kwa kiwango cha lami.

119. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Wizara kupitia TAA kwa kushirikiana na Hazina, imeanza mazungumzo na Serikali ya Canada kuhusu ujenzi wa uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Msalato kupitia Shirika la Biashara la Serikali ya Canada (Canadian Commercial Corporation - CCC). Kwa sehemu kubwa mapendekezo ya mpango wa upatikanaji wa fedha kati ya Hazina na CCC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu na pia kwa upande wa masuala ya kiufundi kati ya CCC na TAA; yamefikiwa. Ni matarajio yetu ujenzi wa uwanja huo utaanza mwaka 2015/2016.

120. **Mheshimiwa Spika**, kiwanja cha ndege cha Arusha ni muhimu katika ukuaji wa sekta ya utalii nchini. Ili kuhakikisha kuwa fursa hii inatumika kikamilifu, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea na maandalizi

ya ukarabati wa kiwanja hiki. Zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya marejeo ya usanifu wa miundombinu ya kiwanja pamoja na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya Mkandarasi zilifunguliwa Machi, 2015. Kazi ya uchambuzi wa zabuni hizi inaendelea.

121. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha na kuboresha huduma na usalama wa viwanja vya ndege nchini katika viwango vya Kimataifa, katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imenunua mitambo mipya minne (4) ya kufua umeme na madaraja matano (5) mapya ya kupandia na kushuka abiria (aerobridges) katika kiwanja cha JNIA. Kazi ya usimikaji wa mitambo hiyo inaendelea. Aidha, kazi ya kusimika kamera za usalama katika viwanja vya ndege vya Songwe na Arusha imekamilika na kazi za usimikaji na uboreshaji wa kamera za usalama katika viwanja vya ndege vya JNIA na Mwanza zinaendelea. Vilevile, Mamlaka ilisimika mitambo kumi (10) yenye mifumo ya teknolojia ya kisasa ya ukaguzi wa abiria na mizigo ili kuimarisha ulinzi na usalama wa usafiri wa anga katika viwanja vya JNIA (4), Songwe (2), Mwanza (1), Dodoma (1) na Bukoba (2).

122. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilianza kazi ya kufunga mashine za kisasa za ukaguzi wa

mizigo zenye uwezo wa kutambua madawa ya kulevya (rapscan x-ray machines 600 series) katika viwanja vya ndege vya Kilimanjaro, Mwanza, Songwe na Arusha.

123. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Mamlaka ilikamilisha kazi za kupima maeneo ya viwanja vipya vya ndege vya Kisumba (Rukwa), Msalato (Dodoma), Omukajunguti (Kagera) na Igegu (Simiyu). Kazi inayoendelea ni ufuatiliaji wa upatikanaji wa hati miliki ya ardhi kwa maeneo hayo.

4.3 Huduma za Usafiri wa Ndege

124. **Mheshimiwa Spika**, huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi ziliendelea kutolewa na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na Kampuni binafsi zikiwemo *Precision Air*, *Fastjet*, *Auric* na *Coastal Air*. ATCL iliendelea kutoa huduma zake katika mikoa ya Mtwara na Kigoma na katika nchi za Burundi na Comoro kwa kutumia ndege yake aina ya Dash 8 Q300 na ndege ya kukodi aina ya CRJ-100.

125. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto zinazoikabili ATCL, Kampuni hii iliendelea kutoa huduma za usafirishaji wa abiria. Katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015, ATCL ilisafirisha abiria 40,090 ikilinganishwa na abiria 41,589 waliosafirishwa

katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014. Hii ni sawa na upungufu wa asilimia 4. Sababu za upungufu huo ni pamoja na ndege aina ya Dash 8 Q300 kuwa kwenye matengenezo makubwa (C-Check). Hivi sasa huduma za usafiri wa ndege zinatolewa kwa kutumia ndege moja ya kukodi aina ya CRJ - 100.

126. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Kampuni ya ATCL imeendelea kuimarisha Chuo chake cha *Air Tanzania Training Institute* ili kuongeza idadi ya watoa huduma za ndani ya ndege nchini. Hadi Aprili, 2014, Chuo kimetoa wahitimu 567. Kati ya hao, asilimia 30 ya wahitimu wamepata ajira katika mashirika ya ndege ya *Precision Air*, *Fastjet*, *Tropical Air* na *Kahama Gold Mining*. Kampuni nyingi binafsi zimeoneka kuvutiwa na wafanyakazi wenye vibali au uzoefu wa fani mbalimbali. Chuo kimekuwa kikiwapatia wahitimu wake mafunzo katika fani zao na kutoa mafunzo ya kompyuta hivyo kuwa kivutio kwa waajiri. Hatua hii imesaidia kuongeza fursa za ajira kwa vijana wa Kitanzania.

127. **Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) umeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kutumia ndege nne (4) kutoa huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Katika mwaka 2014/2015, Wakala uliendelea kuzifanyia matengenezo stahiki ndege zake kulingana na sheria za usalama wa usafiri wa anga na kutoa mafunzo kwa marubani na wahandisi wa ndege zake. Aidha, Wakala uliajiri marubani wanne (wanawake wawili na wanaume wawili). Vilevile jumla ya marubani sita, wahandisi na mafundi Sanifu nane walipatiwa mafunzo.

5.0 HUDUMA ZA HALI YA HEWA

128. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2014/2015, Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) iliendelea kuboresha huduma zake katika maeneo mbalimbali. Maeneo hayo yalihusu utoaji wa huduma, vifaa, utaalum na ushirikiano. Aidha, Mamlaka ilitoa tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa kwa ajili ya usalama wa watu na mali zao.

129. ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuimarisha utabiri wa hali ya hewa na utoaji wa tahadhari ya hali mbaya ya hewa nchini ili kuongeza ufanisi katika shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika Ziwa Victoria, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi ya ufungaji wa rada ya hali ya hewa huko Kiseke, Mwanza ilikamilika Desemba, 2014. Hii ni rada ya pili kufungwa nchini baada ya rada ya kwanza kufungwa Dar es Salaam mwaka

2011. Aidha, ukarabati wa ofisi za kutoa taarifa za hali ya hewa kwa watumiaji walio katika maeneo ya Ziwa Victoria, Mwanza na Ziwa Tanganyika, Kigoma umekamilika na huduma zimeanza kutolewa kupitia Bandari ya Mwanza. Maandalizi ya kutoa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji walio katika maeneo ya Ziwa Tanganyika na Nyasa yanaendelea.

130. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, kupitia miradi ya mabadiliko ya tabia nchi na kupunguza athari zitokanazo na hali mbaya ya hewa, Mamlaka ilinunua mitambo mitano (5) ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe (Automatic Weather Stations). Hatua hii imefanya mitambo ya aina hiyo kufikia 25 nchi nzima ikilinganishwa na hitaji la mitambo 80. Aidha, Mamlaka ilifufua kituo cha kupima hali ya hewa ya anga ya juu (upper air station) huko Tabora. Ufufuaji wa kituo hiki umefanya kuwa na vituo viwili vya aina hiyo nchini ikilinganishwa na hitaji la vituo vinne. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa kuanza ujenzi wa Kituo Kikuu cha Utabiri wa Hali ya Hewa imekamilika. Kazi ya usanifu wa kina inaendelea na inatarajiwa kukamilika Septemba, 2015. Aidha, Mamlaka inaendelea na taratibu za kukarabati ofisi ya Zanzibar ili kuboresha huduma za hali ya hewa. Kazi ya uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano na uchambuzi wa takwimu za hali ya hewa

katika vituo vya JNIA, Zanzibar, KIA, Mwanza na Kituo Kikuu cha Utabiri kilichopo katika Ofisi za Mamlaka zilizoko Ubungo, Dar es Salaam ilikamilika Januari, 2015.

131. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka imeendelea kuboresha uangazi wa hali ya hewa katika Bahari ya Hindi kwa kuanza kutumia maboya maalum ya kupima hali ya hewa. Aidha, maandalizi ya utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa Ziwa Victoria zilikamilika. Maandalizi ya kutoa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa Ziwa Tanganyika na Nyasa yanaendelea. Aidha, uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano na uchambuzi wa *data* za hali ya hewa katika vituo vya JNIA, Zanzibar, KIA, Mwanza na Kituo Kikuu cha Utabiri ulikamilika Januari, 2015.

132. **Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizotekelezwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa katika mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:

- (i) Uboreshaji wa studio ya utoaji wa taarifa za hali ya hewa;
- (ii) Kutoa utabiri wa hali ya hewa kupitia magazeti 5, redio 41, luninga 8, tovuti ya Mamlaka na mitandao mbalimbali ya kijamii; na
- (iii) Kuendelea kutekeleza mfumo wa utoaji huduma bora za hali ya hewa kulingana

na matakwa ya Shirika la Viwango Duniani (ISO). Mamlaka ilifanyiwa ukaguzi Novemba, 2014 ambapo Mamlaka imeendelea kumiliki cheti cha ubora.

133. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kuboresha usambazaji wa taarifa za hali ya hewa kwa watumiaji wakubwa na wadogo. Katika kuboresha usambazaji huo, Mamlaka kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, ilitayarisha mfumo wa ujumbe mfupi kwa Wakulima (Farm SMS) kupitia simu za mkononi. Ujumbe huo unawawezesha wakulima na wafugaji kupata taarifa za hali ya hewa hadi ngazi ya vijijini. Kwa kuanzia, ujumbe huu sasa unasambazwa katika maeneo ya Same, Monduli, Longido, Kiteto, Chamwino, Ngorongoro, Lushoto na Sengerema.

134. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kujijengea heshima Kimataifa katika utoaji wa huduma za hali ya hewa. Katika mwaka 2014/2015, Mamlaka ilizisaidia nchi za Saudi Arabia, Nigeria, Libya, Uganda, Burundi na Rwanda ili kuboresha shughuli za hali ya hewa kwa kutoa utaalam wa aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusaidia uanzishwaji wa mfumo wa usimamizi wa utoaji huduma bora za hali ya hewa kwa

sekta ya usafiri wa anga na utumiaji wa mifumo ya kisasa ya utabiri wa hali ya hewa. Mashirikiano haya yameendelea kuiongezea nchi yetu heshima.

6.0 TAASISI ZA MAFUNZO

135. **Mheshimiwa Spika**, vyuo vilivyo chini ya Wizara vimeendelea kutoa mafunzo katika fani mbalimbali kwa lengo la kuboresha miundombinu na huduma za uchukuzi na hali ya hewa. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Hali ya Hewa - Kigoma, Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC) na Chuo cha Reli Tabora (TIRTEC).

6.1 Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

136. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kiliendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo katika fani za uhandisi wa meli, unahodha, pamoja na utaalum kwenye masuala ya uchukuzi na usafirishaji wa mizigo kwa njia ya bahari na maziwa. Katika mwaka 2014/2015, Chuo kilidahili wanafunzi 92 wa shahada ya kwanza katika fani za uhandisi wa meli na

unahodha. Kati yao wanawake ni sita. Aidha, wanafunzi 176 wa ngazi ya cheti na diploma walidahiliwa wakiwemo wanawake 10.

137. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Chuo kilidahili wahandisi wa meli na manahodha 77, wataalamu wa miundombinu ya upokeaji na usafirishaji mizigo kwa njia ya bahari 142, na wanafunzi 3,672 wa kozi za awali za ubaharia. Ongezeko hili la udahili ni sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 3 ikilinganishwa na mwaka 2013/2014. Aidha, kazi ya kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuboresha madarasa, maabara, karakana na ofisi za waalimu kwenye eneo lililopo mtaa wa Sokoine inaendelea.

138. **Mheshimiwa Spika**, uboreshaji wa Chuo cha Bahari umeendelea kuzingatwa katika mipango ya Wizara ya kila mwaka. Lengo ni kuhakikisha kuwa Chuo hiki kinaendelea kutoa mafunzo kwa kiwango cha Kimataifa. Ili kuendelea kuboresha Chuo hiki, katika mwaka 2014/2015, Chuo kilinunua mtambo wa kufundishia (full mission engine room simulator) kwa gharama ya dola za Marekani 360,000. Usimikaji wa mtambo huu umekamilika na umeanza kutumika Aprili, 2015. Aidha, jumla ya Shilingi bilioni 1.21 zililipwa kwa wakazi 216 wa kitongoji cha Kiparang'anda Wilayani Mkuranga ikiwa ni fidia ya eneo la ekari 500 litakalotumika

kujenga Chuo kipya. Malipo yaliyofanyika ni sawa na asilimia 82.4 ya fedha yote inayohitajika. Ufuatiliaji wa hati miliki na mpango wa matumizi bora ya ardhi unaendelea.

139. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Chuo kinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa walimu hasa walimu wa mabaharia. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Chuo kiliajiri walimu 12. Baadhi ya walimu hao wamekwenda mafunzo kwa vitendo (sea service training) ili wajiendeleze kitaaluma na kukidhi matakwa ya sifa zinazotakiwa. Walimu hao wanaendelea kupata mafunzo katika Kampuni ya meli ya *Danaous* yenye usajili wake Zanzibar. Napenda kutoa shukrani kwa Kampuni hiyo kukubali kutoa nafasi za mafunzo ya vitendo kwa walimu wetu.

140. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kimeanza maandalizi ya uanzishaji wa kozi za usalama katika sekta ya mafuta na gesi baharini. Novemba, 2014 Chuo kiliingia makubaliano ya ushirikiano wa kubadilishana utaalam na mafunzo katika sekta ya mafuta na gesi na Chuo cha *Stavanga Offshore Technical College* cha Norway.

6.2 Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

141. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya

msingi ambayo ni kutoa mafunzo, ushauri elekezi na kufanya tafiti mbalimbali. Aidha, Chuo kiliongeza programu zake hadi kufikia 50 ikilinganishwa na programu 27 zilizokuwepo mwaka 2013/2014. Hili ni ongezeko la asilimia 85. Katika mwaka 2014/2015, Chuo kilidahili wanafunzi 1,688 ikilinganishwa na wanafunzi 1,582 waliidahiliwa katika mwaka 2013/2014. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 7. Kwa sasa, Chuo kina jumla ya wanafunzi 3,248 ikilinganishwa na wanafunzi 2,653 waliokuwepo mwaka 2013/2014. Hili ni ongezeko la wanafunzi kwa asilimia 22.

142. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Chuo kiliendelea na ujenzi wa Kituo Cha Kisasa Cha Ukaguzi wa Magari pamoja na kusimika mtambo mmoja wa ukaguzi wa magari. Hatua hii ni muhimu katika kukabiliana na ajali za barabarani zinazotokana na uchakavu wa magari. Aidha, Chuo kimeingia mkataba na Shirika la Viwango Tanzania wa kukagua magari yaliyotumika na kuingia nchini bila kukaguliwa. Katika kuendelea kukabiliana na tatizo la ajali za barabarani, Chuo kilitoa mafunzo ya muda mfupi wa udereva mahiri kwa washiriki 5,231 ikilinganishwa na washiriki 3,635 waliohudhuria katika mwaka 2013/2014. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 44.

6.3 Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC)

143. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Usafiri wa Anga (Civil Aviation Training Centre - CATC) kimeendelea kutoa mafunzo yanayokidhi viwango vya Kimataifa katika sekta ya usafiri wa anga kwa Watanzania na nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Uganda na Rwanda. Mafunzo yanayotolewa ni ya fani za uongozaji ndege, mawasiliano, usambazaji wa taarifa za safari za ndege, usalama wa viwanja vya ndege na utafiti na ushauri kuhusu usalama wa usafiri wa anga.

144. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, jumla ya wanafunzi 531 walihitimu mafunzo. Kati yao wanafunzi 421 ni Watanzania na 110 ni kutoka nje ya nchi. Aidha, Chuo kimeanza kushirikiana na vyuo vingine vya ndani na nje ya nchi na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) ili kubadilishana mbinu na ujuzi katika uendeshaji wa mafunzo na kozi mbalimbali.

145. **Mheshimiwa Spika**, Oktoba, 2014, Chuo kiliandaa Mkutano Mkuu wa kwanza wa Shirikisho la Vyuo vya Usafiri wa Anga Barani Afrika (Africa Aviation Training Organization - AATO). Mkutano huo ulikuwa ni fursa nyingine ya kuitangaza nchi yetu na vivutio vyake.

6.4 Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma

146. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kuboresha Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma ili kiendelee kutoa mafunzo yenye tija. Katika mwaka 2014/2015, Chuo kilipata usajili wa NACTE unaovuka mipaka ya nchi (cross border registration) na kudahili wanafunzi 31 waliojiunga na mafunzo ya kati ya hali ya hewa. Aidha, wanafunzi 16 walihitimu mafunzo ya kutoa huduma za hali ya hewa katika sekta ya usafiri wa anga. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na ukarabati wa baadhi ya miundombinu ya Chuo na ununuzi wa vitendea kazi muhimu vikiwemo vifaa vya ofisi.

6.5 Chuo cha Reli Tabora (TIRTEC)

147. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Chuo cha Reli Tabora kimeendelea kutoa mafunzo katika fani mbalimbali za huduma ya reli. Chuo hiki kina uwezo wa kuhudumia Wanafunzi 200 katika kampasi ya Tabora na wanafunzi 150 katika kampasi ya Morogoro. Aidha, katika mwaka 2014/2015, Chuo kimeendelea kutoka mafunzo kwa wanafunzi 228 katika kozi za stesheni masta wanafunzi 44; magadi na wakaguzi wa tiketi 38; wakaguzi wa njia ya reli 21; udereva wa treni 33;

wakaguzi wa mabehewa 30; mafundi umeme wa injini 32 na mafundi mitambo wa injini 32. Kwa sasa Chuo cha Reli kimesajiliwa na Baraza la Vyuo vya ufundi (NACTE) na kipo katika mchakato wa kupata udahili wa kudumu (full Accreditation). Mchakato huo unaendelea.

7.0 MASUALA MTAMBUKA

7.1 Kuzingatia Masuala ya Jinsia

148. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa wanawake walioko katika sekta ya uchukuzi wanashirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu yake. Hii ni pamoja na kushiriki katika mikutano na makongamano yahasuyo haki zao. Oktoba, 2014, Wizara ilishiriki katika Kongamano la Kimataifa la Wanawake Wanaojihusisha na Masuala ya Usafiri wa Bahari (Association for Women in Maritime Sector in East and South Africa) lililokuwa na kauli mbiu ya *Build Sustainable Platform of Women in Maritime Sector*. Kongamano hilo pia limeitangaza Tanzania na kukuza uchumi kwani wanawake wa Tanzania walibadilishana mawazo na kufanya biashara na wenzao kutoka nchi mbalimbali. Aidha, kongamano hilo limeonesha

fursa za wanawake wa Tanzania katika sekta ya bahari.

7.2 Utunzaji wa Mazingira

149. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa miradi yote inayotekelezwa katika sekta ya uchukuzi hususan ujenzi wa viwanja vya ndege, reli na miundombinu ya majini inafanyiwa Tathmini ya Mazingira (Environmental Impact Assessment-EIA). Tathmini hizi zimesaidia kuhakikisha kuwa mazingira katika maeneo ambayo miradi hiyo inatekelezwa hayaathiriki.

150. **Mheshimiwa Spika**, hivi sasa Tanzania ina miradi mingi ya utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta. Idadi kubwa ya miradi hii hutekelezwa katika eneo la bahari na nchi yetu imekaribiana na njia kuu ya meli za Kimataifa zikiwemo zile zinazobeba mafuta. Kitendo cha uwepo wa miradi hiyo na kuwa karibu na njia ya meli za Kimataifa, kinaifanya nchi yetu kuwa katika hatari kubwa ya kukumbwa na mlipuko wa moto unaotokana na mafuta. Kutokana na Mikataba ya Kimataifa tuliyoingia kama nchi, tunawajibika kuhakikisha kuwa tunalinda mazingira ya eneo lote la Tanzania ikiwa ni pamoja na maeneo ya karibu na mipaka yetu.

151. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu huo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Taasisi nyingine imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kulinda mazingira ya bahari endapo mafuta yatamwagika. Hatua hizo ni pamoja na kukamilisha Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mafuta Yatakayomwagika Baharini (National Marine Oil Spill Response Contingency Plan - NMOSCP).

152. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu utunzaji wa mazingira katika huduma za usafiri wa reli, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutunza mazingira. Aidha, Wizara imeendelea kuisisitiza matumizi ya kilimo bora kinachozingatia utunzaji wa mazingira. Hii ni pamoja na utunzaji wa mazingira maeneo ambayo shughuli za kijamii zinazofanyika katika milima iliyo karibu na njia ya reli hususan sehemu za Kilosa hadi Gulwe. Shughuli hizo za kibinadamu zinasababisha mafuriko wakati wa mvua na kuathiri huduma za uchukuzi wa reli ya Kati kwa kiasi kikubwa. Naomba kuendelea kuwasihi Waheshimiwa Wabunge, Madiwani na Viongozi wa Serikali katika ngazi za Wilaya, Tarafa, Kata, mitaa na vitongoji kuendelea kuelimisha Wananchi na kukemea vitendo vya kukata miti ovyo, kulima bila kufuata ushauri

wa kilimo bora na kulima kwenye kingo za mito na reli.

153. **Mheshimiwa Spika**, vyombo vya usafiri huchangia katika ongezeko la gesi joto (green house gasses emissions) Duniani. Kwa kutambua athari hiyo, katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na wadau wengine chini ya ufadhili wa UNDP inaendelea kuandaa Hadidu za Rejea za utambuzi wa maeneo yatakayohusishwa kwenye mradi wa kupunguza gesi joto inayotokana na vyombo vya uchukuzi (Nationally Appropriate Mitigation Actions - NAMAS).

154. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano (Serikali ya Mapinduzi Zanzibar – SMZ) kufanya kazi kwa pamoja ili kusimamia usalama wa vyombo vya usafiri majini. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka 2014/2015, tulifanya ukaguzi wa meli za abiria zilizo na umri wa zaidi ya miaka 25. Lengo ni kukagua ubora wa meli hizo na kuangalia kama bado zina uwezo wa kuendelea kutoa huduma. Ukaguzi huo ulibaini kwamba meli hizo zinaweza kuendelea kufanya kazi kwa kipindi kingine cha miaka mitano iwapo zitafanyiwa matengenezo yaliyoainishwa. Meli zilizokaguliwa

ni MV.Maendeleo, MV Serengeti na MV Flying Horse kwa upande wa Zanzibar. Kwa upande wa Tanzania Bara, meli zilizokaguliwa ni za MV.Liemba, MV.Victoria, MV.Serengeti, MV.Butiana, MV.Songea na MV.Iringa.

7.3 Usalama katika sekta ya uchukuzi

155. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia usalama katika utoaji wa huduma za usafiri wa angani na majini. Uwepo wa Bandari zisizo rasmi kimekuwa ni kikwazo katika kuimarisha usalama wa usafiri wa majini na kuathiri mapato ya nchi kwani Bandari hizi hutumika kupitisha mizigo isiyolipiwa kodi za Serikali. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, tarehe 18 Februari, 2015, kilifanyika kikao kilichoishirika Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano (SMZ), Wakuu wa Mikoa na Wilaya zilizo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na Jeshi la Polisi. Agenda kuu ya kikao hicho ilikuwa ni usalama na ulinzi wa usafiri majini ili kutafuta ufumbuzi wa vitendo vya kihalifu vinavyotokea katika maeneo yenye Bandari zisizo rasmi ikiwemo uharamia, biashara haramu ya silaha na binadamu, uhamiaji haramu, ujangili, biashara ya magendo, utumiaji wa vyombo visivyo salama

kubeba abiria na mizigo na hivyo kuhatarisha usalama wa watu na mali. Aidha, Wajumbe wa kikao hicho walikubaliana kufunga matumizi ya bandari zisizo rasmi.

156. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bandari zenye umuhimu kwa wananchi kiuchumi na kijamii, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) na Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) ziliagizwa kurasimisha bandari hizo na kuziweka chini ya uangalizi wa Vijiji vilivyo kwenye maeneo husika. Bandari zitakazorasimishwa zitawekwa katika mpango wa kuboreshwa hatua kwa hatua. Hii itasaidia kupunguza tatizo la uwepo wa bandari bubu katika mwambao wa Tanzania Bara na Zanzibar.

157. **Mheshimiwa Spika**, usalama wa usafiri majini ni suala ambalo ni shirikishi. Hivyo, kupitia Bunge lako Tukufu, nawaomba wananchi kutoa taarifa kwa vyombo vya dola na Serikali za mitaa zilizo karibu nao mara wanapoona aina yoyote ya uvunjifu wa sheria na taratibu za usafiri majini na vitendo vingine haramu ili kuimarisha ulinzi na usalama wa maeneo yao na Taifa kwa ujumla. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa bandari zisizo rasmi katika mwambao wa Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, vikao vya kuimarisha ulinzi na usalama katika mikoja inayopakana na maziwa

ya Tanganyika, Victoria na Nyasa vitafanyika. Lengo ni kupata ufumbuzi wa matatizo ya kuwepo kwa bandari zisizo rasmi kwenye maziwa hayo kitendo kinachoathiri ulinzi na usalama wa nchi na shughuli za kiuchumi na kijamii.

158. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka ya Bandari inaendelea kutekeleza mradi wa kujenga uwezo wa bandari nchini ili kuwa na huduma ya kisasa ya kupokea uchafu (waste reception facilities) kutoka melini. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kutunza mazingira ya bahari, fukwe na meli.

7.4 Udhibiti wa UKIMWI

159. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kupima ili kujua afya zao. Watumishi waliotambuliwa kuwa na maambukizi ya UKIMWI na wanaoishi na virusi vya UKIMWI waliendelea kupatiwa huduma kwa kuzingatia mwongozo uliopo. Suala la kukabiliana na UKIMWI limekuwa agenda mojawapo katika mikutano ya Wafanyakazi. Hii imesaidia kuwakumbusha wafanyakazi kuhusu umuhimu wa kuchukua tahadhari. Aidha, Wataalam wa afya wameendelea kualikwa ili kutoa elimu ya kujikinga pamoja na jinsi ya kuishi na virusi vya UKIMWI.

7.5 Mapambano Dhidi ya Rushwa

160. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliunda upya Kamati ya maadili baada ya wajumbe wa Kamati ya awali kuhama na wengine kustaafu. Kamati hiyo imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha uzingatiaji wa maadili kwa kuandaa Mpango Kazi wake. Aidha, Wizara na Taasisi zimeendelea kuhimiza wafanyakazi kuepuka vitendo vya rushwa na uzingatiaji wa maadili na utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma. Suala hili pia limeendelea kusisitizwa katika vikao vya Watumishi katika ngazi mbalimbali. Katika mwaka 2014/2015, Watumishi waajiriwa wapya na wale waliohamishiwa kwenye Wizara hii walipewa mafunzo ya madili na mafunzo mahsusi yanayoelekeza kujiepusha na vitendo vya kutoa au kupokea rushwa. Watumishi hao pia walifanyiwa zoezi la kuweka tamko rasmi linalowataka kuzingatia maadili ya Utumishi wa Umma.

7.6 Habari, Elimu na Mawasiliano

161. **Mheshimiwa Spika**, Wizara na taasisi zilizo chini yake imeendelea kuelimisha Umma

wa Watanzania kwa kuwapatia taarifa za programu na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wizara kupitia tovuti, ziara, mikutano, vyombo mbalimbali vya habari na kushiriki katika maonesho mbali mbali ya Kitaifa. Mwaka 2014/2015, Wizara ilishiriki kwenye kipindi cha *Tembea Uone* kinachoandaliwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), kilichoonesha na kuelezea mada mbali mbali za mafanikio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Mada hizo ni pamoja na uboreshaji na uimarishaji wa miundombinu ya reli na vifaa vitembeavyo juu ya reli, viwanja vya ndege, usafiri wa anga, Hali ya hewa na bandari.

162. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara na Taasisi zilizo chini yake iliendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:

- (i) Kuchelewa kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na kutopatikana fedha kwa wakati na kwa kiwango kilichoidhinishwa;
- (ii) Kushindwa kupata wawekezaji mahiri kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya sekta hususan reli na bandari;

- (iii) Kuendelea kuwepo kwa ajali katika usafiri wa barabara, reli na majini ambazo zinachangia kupoteza maisha ya wananchi na mali zao;
- (iv) Uharibifu na hujuma ya miundombinu ya reli, vitendea kazi na vifaa mbalimbali kutokana na biashara ya vyuma chakavu;
- (v) Michango ya Washirika wa Maendeleo kutopatikana kwa wakati na au kutolewa chini ya kiwango walichoahidi;
- (vi) Msongamano wa magari jijini Dar es Salaam na malori kwenye barabara zinazolingia bandarini na hivyo kupunguza ufanisi wa bandari; na
- (vii) Serikali kutumia fedha nyingi kutokana na uharibifu wa miundombinu ya uchukuzi unaosababishwa na uharibifu wa mazingira na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

8.0 MALENGO YA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KATIKA MWAKA 2015/2016

8.1 Miradi Itakayotekelezwa Katika Mwaka 2015/2016 Chini ya Mpango wa BRN

163. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa bandari ya Dar es salaam, kazi za zitakazotekelezwa katika mwaka 2015/2016 ni pamoja na:

- i. Kuanza kazi ya kuongeza kina na kupanua lango la kuingilia na eneo la kugeuzia meli katika Bandari ya Dar es Salaam;
- ii. Kuanza uboreshaji wa gati Na. 1 – 7 katika Bandari ya Dar es Salaam;
- iii. Kukamilisha mradi wa TEHAMA wa kuwaweka pamoja watoa huduma (Electronic Single Window System); na
- iv. Kukamilisha mradi wa mfumo wa usalama Bandarini (Integrated Security System).

164. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia MSCL itaanza ujenzi wa meli mbili mpya; moja (1) katika Ziwa Victoria na nyingine katika Ziwa Tanganyika. Aidha, kazi ya ukarabati wa meli za MV.Umoja, MV.Victoria na MV.Serengeti katika Ziwa Victoria itafanyika. Kazi nyingine zitakazotekelezwa katika kipindi hicho ni pamoja na kuweka mfumo mpya wa kielektroniki wa kukata tiketi, kulipa madeni ya watoa huduma na kulipia bima za meli hizo.

165. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia sekta ndogo ya reli imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kukamilisha usanifu wa kina wa ujenzi wa reli kati ya Tabora – Kigoma, Uvinza - Musongati na Kaliua – Mpanda – Karema;
- (ii) Kuanza ujenzi wa reli kutoka Dar es salaam – Isaka – Keza – Kigali/Musongati (Km 1600);
- (iii) Kujenga madaraja yaliyo chini ya uwezo wa tani 25 kwa ekseli;
- (iv) Kufanya usanifu na kuanza ujenzi wa madaraja 16 kati ya 25 yaliyo katika hali mbaya kati ya Dar es Salaam – Tabora;

- (v) Kufanya usanifu na ujenzi wa mabwawa 2 ya *punguza* katika maeneo ya Kimagai na Msagali;
- (vi) Kuunda upya vichwa vingine 9 katika karakana ya reli iliyoko Morogoro;
- (vii) Kununua mabehewa mengine mapya ya abiria 22;
- (viii) Kuunda upya vichwa 3 vya *sogeza* vyenye uwezo mkubwa;
- (ix) Kununua viberenge 5 kwa ajili ya ukaguzi wa njia;
- (x) Kuanza ujenzi wa daraja (Km 349/5c) kati ya stesheni za Godegode na Gulwe;
- (xi) Kufanya matengenezo ya kawaida ya njia ya reli; na
- (xii) Kuanza ulipaji wa fidia wa eneo la Buhongwa kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya kupanga mabehewa na kugeuzia treni (marshalling yard).

8.2 Miradi Itakayotekelezwa Katika Mwaka 2015/2016 Nje ya Mpango wa BRN

166. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia SUMATRA itamtafuta Mshauri Mwelekezi wa

kufanya utafiti wa kina kuhusu vyanzo, madhara na namna bora ya kukabiliana na msongamano katika miji na majiji yetu.

167. **Mheshimiwa Spika**, huduma za reli ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote. Kwa kuzingatia umuhimu huu, jitihada zinazoendelea baina ya nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda katika ujenzi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka – Keza – Kigali/Musongati kwa kiwango cha Kimataifa na kwa kutambua kuwa sehemu kubwa ya reli hiyo iko upande wa Tanzania, RAHCO ilimwajiri Mtaalam Mshauri (Transaction Advisor), Kampuni ya *Rothschild* kwa ajili ya kuandaa mradi huo kwa upande wa Tanzania. Mtaalam Mshauri huyo alianza kazi Machi, 2015 na anatarajiwa kukamilisha Juni, 2016. Aidha, RAHCO inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za uendelezaji wa mradi huo kiasi cha Dola za Marekani bilioni 7.6 kutoka katika mabenki na taasisi mbalimbali za kifedha. Mpango uliopo ni kujenga reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa ndani ya ukanda wa reli ya sasa kuanzia mwaka ujao wa fedha. Mradi huu utahusisha ujenzi wa reli mpya kwa kiwango cha Kimataifa kati ya Dar es Salaam hadi Kigoma; Tabora hadi Mwanza; Kaliua hadi Mpanda na Mpanda hadi Karema; na ujenzi wa reli mpya kati ya Uvinza

hadi mpakani na Burundi kwa kuzingatia upembuzi yakinifu na usanifu wa reli hiyo.

168. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, RAHCO inatarajia kuanza ujenzi wa reli ya Mtwara – Songea – Mbamba Bay pamoja na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga (Km 1000) na reli ya Tanga – Arusha – Musoma kwa kiwango cha Kimataifa.

169. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa TAZARA, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na kuendelea kufanya usanifu wa kina wa ujenzi wa matawi ya reli za Kiwira – Uyole - Itungi (Km 75), Mlimba - Liganga – Mchuchuma – MbambaBay (Km 260), Tunduma – Sumbawanga – Kigoma (Km 700) na tawi la reli kwenda Bandari ya Kasanga. Miradi mingine itakayotekelezwa ni uimarishaji wa miundombinu ya njia kuu ya reli, ukarabati wa vichwa vya treni, mabehewa ya mizigo, abiria, mitambo, mashine na vifaa vya usalama; kukarabati karakana iliyoko Dar es salaam na kukarabati mitambo ya kiwanda cha kuzalisha kokoto na mataruma cha Kongolo, Mbeya.

170. **Mheshimiwa Spika**, Kampuni inayomilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China (SINOTASHIP) itakodi meli moja ya mizigo (charter-in) kutoka

Kampuni washirika ya *China Ocean Shipping Company* (COSCO) ya China ili kuongeza ufanisi wa Kampuni na kutafuta fedha ili kujenga meli ya mizigo na kukamilisha utafiti wa kununua meli ya kusafirisha gesi (LNG).

171. **Mheshimiwa Spika**, kazi za uendelezaji wa huduma za bandari zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- (i) Kuendelea na ujenzi wa magati katika Ziwa Victoria, Tanganyika, na Nyasa;
- (ii) Kukamilisha ujenzi wa gati la Nyamisati – Rufiji; Kuanza ujenzi wa Bandari ya Mbegani (Bagamoyo);
- (iii) Kuendeleza Bandari mpya ya Mwambani - Tanga;
- (iv) Kuanza ujenzi wa mradi wa kupanua Bandari ya Mtwara kwa kujenga gati mpya nne kwa utaratibu wa Sanifu, Jenga na Gharamia;
- (v) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa kuendeleza bandari zilizo katika Ziwa Victoria na Tanganyika;
- (vi) Kufanya upembuzi yakinifu (economic viability) wa ujenzi wa

bandari za Lindi, Kilwa na Rushungi;
na

- (vii) Kuendelea na ununuzi wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuhudumia mizigo katika bandari zote.

172. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TCAA itanunua rada mpya 2 za kuongozea ndege za kiraia lengo likiwa ni kuendelea kulifanya anga la Tanzania kuwa salama. Aidha, Wizara kupitia TCAA imepanga kufunga mitambo ya kuboresha mawasiliano kati ya waongoza ndege na marubani wakiwa angani (VHF area cover relay station) katika vituo vya Lokisale mkoani Arusha na Mafinga mkoani Iringa ili kuboresha mawasiliano ya anga.

173. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mfuko wa Mafunzo ya Marubani na Wahandisi wa Ndege itafadhili mafunzo ya wanafunzi 10 kwa lengo la kupunguza pengo la uhaba wa marubani na wahandisi wa ndege unaoikabili nchi. Kazi nyingine zitakazotekelezwa na Wizara kupitia TCAA ni kuendelea kukamilisha mfumo mpya wa teknolojia ya ufuatiliaji safari za ndege (Automatic Dependent Surveillance – Broadcast - ADS-B) katika anga la Tanzania ambapo awamu ya kwanza inahusisha takribani nusu ya nchi hadi juu ya bahari ya Hindi; kuendelea

kukamilisha awamu ya pili ya mradi wa kubainisha alama (coordinates) za viwanja vya ndege vya Arusha, Kigoma, Mafia, Lindi, na Tabora kwa kutumia mfumo wa satelaiti (WGS 84); kufunga mtambo mpya wa kusambaza mawasiliano vituoni na kwenye ndege kwa ajili ya viwanja vya ndege vya JNIA, KIA na Abeid Amani Karume na kufunga mitambo mipya ya *ATM EUROCAT* katika kiwanja cha ndege cha JNIA.

174. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Kampuni ya Ndege (ATCL) itakamilisha Mpango Biashara wa Miaka Mitano wa kampuni ya ATCL. Aidha, taratibu za ununuzi wa ndege mbili aina ya Dash 8 Q400 kutoka Kampuni ya *Bombardier* ya Canada zinakamilishwa. Ndege hizo zitanunuliwa kwa mkopo kutoka Benki ya Rasilimali ya Tanzania (TIB). Ndege hizo zinatarajiwa zitawasili Julai, 2015. Hatua hii itaipa ATCL uwezo wa kuhudumia abiria wa ndani na nje na hivyo kuweza kushindana katika soko.

175. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TAA itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo jipya la abiria, maegesho ya ndege na maegesho ya magari katika kiwanja cha JNIA;

- (ii) Kuendelea na ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro;
- (iii) Kukamilisha ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe (Mbeya);
- (iv) Kuanza awamu ya pili ya ukarabati wa viwanja vya ndege vya Kigoma na Tabora;
- (v) Kuanza ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Sumbawanga na Shinyanga;
- (vi) Kukamilisha ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Bukoba;
- (vii) Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kiwanja cha ndege cha Mtwara;
- (viii) Kuanza ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Msalato, Dodoma;
- (ix) Kukamilisha kazi za uboreshaji wa kiwanja cha ndege cha Mwanza itakayohusisha ujenzi wa jengo jipya la abiria, eneo la kuegesha ndege pamoja na kurefusha njia ya kuruka na kutua ndege;
- (x) Kukamilisha kazi ya kufunga mashine za kisasa za ukaguzi wa mizigo zenye uwezo wa kutambua madawa ya kulevya (Rapsan x-ray machines 600 series) katika viwanja vya ndege vya

Kilimanjaro, Mwanza, Songwe na Arusha; na

Kufanya marejeo ya usanifu wa jengo jipya la abiria katika kiwanja cha ndege cha Mafia, barabara ya kuingia kiwanjani hapo na maegesho ya magari pamoja na kufukia eneo lililoharibiwa na mvua ili kulinda miundombinu ya kiwanja hicho.

176. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Hali ya Hewa itaboresha miundombinu ya Chuo cha Hali ya Hewa, kuanza ujenzi wa jengo la Kituo Kikuu cha utabiri wa hali ya hewa nchini, ukarabati wa vituo vya hali ya hewa na utekelezaji wa programu ya Taifa ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi. Aidha, Mamlaka ya Hali ya Hewa itaendelea kukarabati miundombinu ya Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma ili kukabiliana na uchakavu wa miundombinu.

177. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kitanunua mitambo ya karakana kwa ajili ya kuendeshea mafunzo ya uhandisi wa meli; kuendeleza miundombinu ya eneo la Chuo pamoja na kuendelea na awamu ya pili ya mradi wa kituo cha mafunzo yanayohusu sekta ya mafuta na gesi baharini (Off-shore Training Centre).

178. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kitaendelea na ujenzi wa kituo cha rasilimali mafunzo (maktaba), ujenzi wa kituo cha kisasa cha ukaguzi wa magari, ukarabati wa majengo ya Chuo, ununuzi wa vifaa vya kufundishia pamoja na ununuzi wa kiwanja mkoani Dodoma kwa ajili ya mafunzo ya anga.

9.0 SHUKRANI

179. **Mheshimiwa Spika**, natoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wote wa sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa kwa ushirikiano waliotoa katika kufanikisha malengo na mipango ya sekta hizo. Wadau hao ni pamoja na Washirika wa Maendeleo waliochangia katika kuhakikisha kuwa mipango na programu zetu zinafanikiwa. Shukrani hizi pia ziwafikie nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyojitokeza katika kuchangia uendelezaji na uboreshaji wa miundombinu na huduma za uchukuzi na hali ya hewa. Nchi na mashirika hayo ni pamoja na Shirika la Bahari Duniani (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), UNESCO, Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi kwa Afrika (BADEA), Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF), Kuwait Fund, Malaysia, Jamhuri ya Korea, OPEC Fund, Umoja wa Nchi

za Ulaya, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), TMEA, DFID, India, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani, Urusi, Sweden, Ufaransa, Finland, Singapore na wengine wengi. Tunaendelea kuomba ushiriki wao katika kukuza uchumi wa nchi na kuimarisha miundombinu na huduma za uchukuzi na hali ya hewa.

180. **Mheshimiwa Spika**, kabla sijahitimisha hotuba yangu, niruhusu niwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Uchukuzi kwa ushirikiano walionipa katika kipindi hiki kifupi tangu nihamie katika Wizara. Viongozi hao ni Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba (Mb.), Katibu Mkuu Dkt. Shaaban Ramadhan Mwinjaka, Naibu Katibu Mkuu, Bi. Monica Lyander Mwamunyange, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi za SUMATRA, TCAA, TGFA, TTFA, KADCO, TAA, TPA, TRL, RAHCO, MSCL, TMA, SINOTASHIP, ATCL, DMI, NIT na TAZARA, viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi. Tangu nilipoanza kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii, ninakiri kupata ushirikiano mkubwa katika kuendeleza miundombinu na huduma za uchukuzi na hali ya hewa. Ahsanteni sana.

10.0 MAOMBI YA FEDHA

181. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kuwa, katika mwaka 2015/2016, Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya Shilingi **452,966,426,000**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **160,433,834,000** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **292,532,592,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Shilingi **54,288,680,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **106,145,154,000** fedha za Matumizi Mengineyo (OC). Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha Shilingi **160,000,000,000** fedha za ndani na Shilingi **132,532,592,000** fedha za nje.

182. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Mafanikio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 (**Kiambatisho Na.1**) na Miradi itakayotekelezwa katika mwaka 2015/2016 (**Kiambatisho Na.2**) ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

183. **Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa napenda kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kunisikiliza wakati

nikiwasilisha Hotuba yangu. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara www.uchukuzi.go.tz.

184. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

KIAMBATISHO NA.I

MUHTASARI WA MAFANIKIO YA SERIKALI KATIKA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 - 2015.

Muhtasari wa mafanikio yaliyopatikana katika Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 – 2015 katika Sekta ndogo za usafiri wa Reli, Majini, Anga na Hali ya Hewa ni kama ifuatavyo:-

I.0 Sekta ya Reli

- i. Mradi wa kutandika reli za ratili 80 kwa yadi kati ya stesheni za Kitaraka na Malongwe (km 89) ulikamilika Februari 2014. Kukamilika kwa ujenzi wa njia ya reli hiyo kunafanya reli zilizotandikwa zenye uzito wa ratili 80 kwa yadi kati ya Dar es Salaam na Tabora kufikia jumla ya km 527.
- ii. Kazi ya kujenga madaraja mawili ya reli (km 303 na km 293) kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe na daraja moja lililopo kati ya stesheni za Bahi na Kintinku umekamilika.
- iii. Kazi ya upembuzi wa kina wa ujenzi wa reli mpya ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali/Musongati ilikamilika Aprili, 2014. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa reli kwa kiwango cha Kimataifa (standard gauge) kutoka Isaka – Mwanza imekamilika. Mshauri Mtaalam (Transaction Advisor) alianza kazi ya kuandaa mradi (packaging for bankability) Septemba, 2014 na kazi inaendelea;
- iv. Kazi ya usanifu wa ujenzi wa daraja jipya na matengenezo ya kuzuia tatizo la mafuriko na uharibifu wa miundombinu ya reli inayotokea mara kwa mara kati ya Gulwe na Godegode ilikamilika Machi, 2015;
- v. Kazi ya kuondoa reli nyepesi na zilizochakaa zenye uzito wa ratili 45 kwa yadi na kuweka reli zenye uzito wa ratili 56.12

kwa yadi kwa umbali wa km 9 zilizobainishwa kuhitaji ukarabati wa haraka kati ya sehemu ya Lumbe - Mto Ugala - Katumba ilikamilika Februari, 2014;

- vi. Kazi ya ununuzi wa vichwa vya treni vipya 7; mabehewa mapya ya mizigo 197; mabehewa ya abiria mapya 22; mitambo mipya ya kunyanyua mizigo mizito 2; vipuri kwa ajili ya matengenezo ya vichwa vya treni 6 na mabehewa; ukarabati wa vichwa vya treni 6 vya sogeza; ukarabati wa mitambo ya kunyanyua mizigo (gantry crane) 4; ukarabati wa vichwa vya treni 6 na vitatu vya sogeza kwa upande wa TAZARA imekamilika.
- vii. Kazi ya kufanya usanifu wa kina wa uboreshaji wa reli ya kutoka Tanga – Arusha imekamilika Mei, 2015;
- viii. Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari mpya ya Mwambani ulikamilika Agosti, 2012. Serikali imeamua kurejea upya upembuzi yakinifu kwa lengo la kuiboresha taarifa hiyo na kujumuisha matarajio ya shehena inayotokana na ugunduzi wa *Soda ash* na *Iron ore*;
- ix. Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Arusha - Musoma pamoja na matawi ya kuelekea Engaruka, Minjingu na Dutwa kwa kiwango cha Kimataifa ilianza Septemba, 2013 na inategemewa kukamilika Agosti, 2015;
- x. Mshauri Mwelekezi wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali ujenzi wa reli ya Mtwara – Songea – MbambaBay (km 1000) na matawi yake ya kwenda Mchuchuma na Liganga kwa kiwango cha kKimataifa alianza kazi Julai, 2014 na kazi hiyo itakamilika Julai, 2015.

2.0 Sekta ya Majini

- i. Kazi ya kuondoa mchanga uliotuama Bandari ya Kigoma ilikamilika Februari, 2012;
- ii. Ukarabati wa Chelezo katika Bandari ya Kigoma ulikamilika Septemba, 2011;

- iii. Kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa namna ya kuboresha miundombinu ya Bandari za Ziwa Victoria itakamilika Mei, 2015;
- iv. Ujenzi wa boya la Mafuta (SPM) ulikamilika na kuanza kutumika Novemba, 2012;
- v. Ununuzi wa vifaa vya kisasa vya *Mobile Harbour crane (MHC) 4; Spreaders for MHC 4; Semi-Automatic Spreaders 12; Highway tractors 6; Reach stakers 3; Empty container Handlers 3 na Terminal tractors 12* umekamilika;
- vi. Kazi za upembuzi yakinifu wa kubaini njia bora ya kuimarisha gati namba I-7, utafiti wa ujenzi wa gati la kuhudumia meli za magari (RoRo) na ujenzi wa 'Conveyor system' na 'Silo' kwa ajili ya kuhudumia shehena ya kichele zilikamilika Desemba, 2012;
- vii. Kazi ya Upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mtwara ilikamilika Oktoba, 2012. Zabuni za ujenzi wa magari manne mapya katika Bandari hiyo zilifunguliwa Novemba, 2014. Ujenzi unatarajiwa kuanza Mei, 2015 na kukamilika mwaka 2018.
- viii. Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari mpya Bagamoyo ulikamilika mwaka 2010. Aidha, kazi ya kufanya tathmini ya fidia zimekamilika na taratibu za malipo zinaendelea kukamilishwa. Ujenzi wa Bandari hii unatarajiwa kufanyika kwa ubia kati ya Serikali za Tanzania, China na Oman. Majadiliano ya namna ya kujenga Bandari hii kati ya wabia hawa yanaendelea. Timu ya wataalam yenye wajumbe kutoka pande zote imeundwa na inaendelea na kazi;
- ix. Ujenzi wa gati la Mafia ulikamilika Septemba, 2013;
- x. Ujenzi wa gati la Kiwira katika Ziwa Nyasa ulikamilika Machi, 2015;
- xi. Ujenzi wa gati la Kipiri katika Ziwa Tanganyika ulikamilika Septemba, 2014;
- xii. Ujenzi wa gati la Kabwe ulikamilika Aprili, 2015;

- xiii. Mkataba wa ujenzi wa gati la Kagunga katika Ziwa Tanganyika ulisainiwa Aprili 2015 na kazi zitaanza Juni, 2015;
- xiv. Ujenzi wa gati la Pangani ulianza Septemba, 2014.

3.0 Sekta ya Anga

- i. Kazi ya ujenzi wa jengo la tatu la abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) ilianza Januari, 2014. Awamu ya kwanza inatarajiwa kukamilika Oktoba, 2015;
- ii. Ujenzi wa Jengo la Watu Mashuhuri katika Kiwanja cha Ndege cha JNIA ulikamilika Oktoba, 2010.
- iii. Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe ulikamilika na kuanza kutoa huduma za uendeshaji wa ndege Desemba, 2012. Kazi ya ujenzi wa jengo la abiria inaendelea;
- iv. Ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha ndege cha Mafia kwa kiwango cha lami ulikamilika Julai 2013;
- v. Awamu ya kwanza ya uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Kigoma na Tabora ilikamilika Juni, 2013;
- vi. Kazi ya ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha Ndege cha Mpanda ilikamilika Machi, 2012;
- vii. Kazi ya ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Arusha kwa kiwango cha lami ilikamilika Juni, 2012.

4.0 Sekta ya Hali ya Hewa.

Ununuzi wa Rada mbili za hali ya hewa kati ya rada saba zinazohitajika umekamilika. Rada ya kwanza ilifungwa Aprili, 2011 Jijini Dar es Salaam na rada ya pili ilifungwa Mwanza Desemba, 2014.

KIAMBATISHO NA.2

Mgawanyo wa Fedha za Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka 2015/2016

Na. Mradi	Jina la Mradi	Kiasi kilichoidhinishwa kwa mwaka 2015/2016 (Tsh. Million)			Chanzo cha Fedha
		Fedha za ndani	Fedha za Nje	Jumla	
1	2	3	4	5 (3+4)	6
KIFUNGU 1003: SERA NA MIPANGO					
6267	Institutional Support				
	i. MOT	500	219.57	719.57	GoT/EU
	ii. Revamping ATCL	1,000	0	1,000	GoT
	iii. Rehabilitation of the existing fleet and contractual liabilities (MSCL).	5,400	0	5,400	GoT
	iv. DMI Training Equipment	950	0	950	GoT
	v. Acquisition of 2 Civil Aviation Radar	12,000	0	12,000	GoT
	JUMLA NDOGO	19,850	219.57	20,069.57	

KIFUNGU 2005: MIUNDOMBINU YA UCHUKUZI					
4156	Construction of Kigoma Airport	400	10,812	11,212	GoT /EIB
4157	Construction of Mafia Airport	1,500	-	1,500	GoT
4159	Construction of Tabora Airport	200	15,017	15,217	GoT/IDA/EIB
4206	Construction of Songwe Airport	5,000	-	5,000	GoT
4209	Construction of Mwanza Airport	7,750	3,028	10,778	GoT/BADEA
4210	Construction of Arusha Airport	100	-	100	GoT
4211	Improvement of TAZARA Railway	1,000	-	1,000	GoT
4213	Relaying of Central Line with 80 pounds per Yard				
	(i) Relaying with 80lbs/yd materials 197kms of track central line (Tabora - Lulanguru) (61 km)	3,000	-	3,000	GoT/IDA
	(ii) Rehabilitation Tura Quarry	1,000	-	1,000	GoT
	(iii) Procurement of Track measuring car and one Motor Trolley	0	4,100	4,100	GoT
	(iv) Beaconing of the Railway Corridor and Station's adjoining land (27,070 poles)	100	-	100	GoT

	(v) Survey and Registration of Railway Plots including all stations	300	-	300	GoT
	(vi) Relaying of track portions with light overstretched and worn out track metal - (Dar - Kilosa 283kms) (Tabora - Isaka, 130 kms)	1,270	24,821	26,091	GoT/IDA
	RAIL REHABILITATION - BRANCH LINES - RAHCO				
4215	(i) Rail Rehabilitation (Kaliua/Mpanda Railways line), design and Construction of Culvert km 154+8 , kms 174 and kms 185	1,000	0	1,000	GoT
	(ii) Design and Construction of station and Goodshed buildings at Mpanda	500	0	500	GoT
	Rail Rehabilitation - Main Line - RAHCO				
4216	(i). Track repair and improvement of drainage Kilosa-Gulwe	2,000	-	2,000	GoT/IDA
	(ii) Realignment Study to avoid Flood prone areas Kilosa - Gulwe	3,000	-	3,000	GoT/IDA
	(iii). Rating and redesign of Bridges to 25 tons per axle load and construction Bridge at Godegode	1,000	2,000	3,000	GoT/IDA

	(iv). Design and Construction of proposed 16 out of 25 No. Condition "E" Culverts and bridges between Dar and Tabora Upgrading and Replacement of low axle load bridges and culverts	230	20,463	20,693	GoT/IDA
	(v) Improve telecommunication system in two phases (Dar-Dodoma, Tabora-Kigoma/ Tabora-Mwanza	1,000	1,000	2,000	GoT/IDA
	(vi) Re-establish cargo tracking system	1,000	-	1,000	GoT
	(vii) Restoration of Railways lines during emergencies	1,000	-	1,000	GoT
	Tabora-Kigoma, Isaka - Mwanza Railway Project				
	(i) Tabora -Kigoma & Kaliua - Mpanda (DD)	2,500	0	2,500	GoT
	(ii) Isaka - Mwanza SG (DD)	700	0	700	GoT
4217	(iii) Feasibility Study and Preliminary Design of Proposed New lines Uvinza-Musongati & Mpanda -Karema	2,000	0	2,000	GoT
	(vi) Land Acquisition at Buhongwa Marshalling Yard	1,000	0	1,000	GoT
	(v) Acquisition of land from Mpanda to Karema for the Proposed New Mpanda to Karema corridor	200	0	200	GoT

4218	Mtwara -Mbambabay, Liganga and Mchuchuma Railway	2,000	0	2,000	GoT
4220	Construction of Mtwara Airport	600	0	600	GoT
4221	Construction of Sumbawanga Airport	3,500	12,207	15,707	GoT/EIB
4222	Construction of Shinyanga Airport	600	13,304	13,904	GoT/EIB
4223	Tanga(Mwambani)-Arusha-Musoma Railway Project				
	(i) Tanga - Arusha (DD)	2,000	0	2,000	GoT
	(ii) Arusha - Musoma, Spurs Minjingu (Engaruka) (FS)	2,000	0	2,000	GoT
	(iii) Revival of Northern Line (Tanga - Arusha)	1,200	0	1,200	GoT
4224	Construction of KIA Airport	50	10,409	10,459	GoT/ORIO
4281	DSM -Isaka -Kigali-Keza-Msongati (DD)	300	0	300	GoT
4282	Inland Container Depots.				
	(i) Mwanza - Shinyanga (ICD)	400	0	400	GoT
	(ii) Remodeling of Intermodal Exchange Terminals of Dar Port rail layouts, Ilala Yard and Isaka ICD's	0	3,137	3,137	IDA
4286	Construction of Msalato Airport	100	0	100	GoT
4287	Construction of Bukoba Airport	200	0	200	GoT/IDA

4289	Construction of Terminal III JNIA	1,000	12,016	13,016	GoT/HSBC
6520	Dev. Of Sea and Inland Berths	50	0	50	GoT
	JUMLA NDOGO	52,750	132,313	185,063	
KIFUNGU 2006: HUDUMA ZA UCHUKUZI					
4219	DSM City Commuter Train Project		0		
	(i) Study of New railway lines	1,900	0	1,900	GoT
	(ii) Construction of extension of Ubungo line loop at Ilala block post to DSM station line to avoid interference of commuter and freight trains from Pugu	500	0	500	GoT
4290	TMA Radar, Equipment and Infrastructure	2,900	0	2,900	GoT
4291	Government Aircrafts maintenance	5,000	0	5,000	GoT
4292	Procurement and repair of Rolling Stock, Equipment and track maintenance	75,100	0	75,100	GoT
6377	Construction and Rehab. of NIT buildings	2,000	0	2,000	GoT
	JUMLA NDOGO	87,400	0	87,400	
	JUMLA KUU	160,000	132,532	292,532	